JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2024

June, 2025

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024

Imetayarishwa na
Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya,
S.L.P 80327, 8 Barabara ya Kivukoni,
11486 Dar es Salaam, **Simu:** +255 22 2113757/54,
Nukushi: +255 22 2113752 **Barua pepe :** cg@dcea.go.tz
Tovuti : www.dcea.go.tz, **Instagram :** @dceatanzania
Twitter : @dceatanzania, **Facebook :** dcea_tz
YouTube: DCEATV Simu ya bure: 119

ISBN:978-9912-9896-5-8

Imetayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Na. 5 ya mwaka 2015)

YALIYOMO

MAELEZO YA WAZIRI vi

DIBAJI vii

FAHARASA viii

SURA YA KWANZA 1

HALI YA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Duniani 1

1.2.1 Bangi 2

1.2.1.1 Uhalalishaji wa Bangi na Athari zake 2

1.2.2 Dawa za Kulevya Jamii ya Afyuni 3

1.2.3 Hali ya Biashara na Matumizi ya Cocaine Duniani 4

1.2.4. Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya 4

1.2.5 Dawa za Kulevya Jamii ya Amphetamine (Amphetanine Type stimulants - ATS) 5

1.2.6 Dawa Mpya za Kulevya (New Psychoactive Substances- NPS) 5

1.3 Dawa za kulevya na jinsia (matumizi ya dawa za kulevya na wanawake) 6

1.4 Dawa za kulevya na Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia 6

SURA YA PILI 7

MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI 7

2.1 Utangulizi 7

2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction) 7

2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction) 7

2.4 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction) .. 8

2.5 Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa 8

SURA YA TATU 9

UDHIBITI WA UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA 9

3.1 Utangulizi 9

3.2 Udhibiti wa Upatikanaji wa Dawa za Kulevya 9

3.2.1 Bangi 9

3.2.2 Mirungi 9

3.2.3 Heroin 12
3.2.4 Cocaine 12
3.2.5 Dawa Nyingine za Kulevya 15
3.2.5.2 Bangi aina ya 'Skanka' na 'Hashish' 15
3.2.5.3. Mescaline 16
3.2.5.4 Methylene-dioxy-pyrovalerone (MDPV)........ 16
3.4 Kuzuia Uchepushwaji wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya 18
3.4.1 Kemikali Bashirifu (Precursor Chemicals)........ 18
3.4.1.1 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu kupitia Mifumo ya Kielektroniki 18
3.5 Udhibiti wa Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya 20
3.6 Ukaguzi wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya........ 20
3.7 Raia wa Kigeni waliokamatwa Nchini 20
3.8 Raia wa Tanzania waliokamatwa nje ya Nchi 21
3.9 Kesi za Dawa za Kulevya........ 21
3.10 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya na Kemikali Bashirifu 21
3.11 Maboresho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Sura ya 95 23

SURA YA NNE 24
KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA (DEMAND REDUCTION)........ 24
4.1 Utangulizi 24
4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya 24
4.2.1 Matumizi ya Dawa za Kulevya kwenye Shisha 24
4.2.2 Uchanganyaji wa Dawa haramu za Kulevya kwenye Shisha........ 25
4.2.3 Sheria inasemaje kuhusu kuchanganya dawa za kulevya kwenye Shisha? 26
4.3 Sababu zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya 26
4.4 Madhara ya Dawa za Kulevya........ 28
4.4.1 Kiafya........ 28
4.4.2 Kijamii 28
4.4.3 Kiuchumi........ 29
4.4.4 Kisiasa/Kidiplomasia........ 29
4.4.5 Kimazingira........ 29
4.5 Jitihada zilizofanyika katika Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya........ 29
4.5.1 Kazi za Uelimishaji Zilizofanywa na Mamlaka........ 30

4.5.2 Uelimishaji uliofanywa na Asasi za Kiraia 33

SURA YA TANO 34

KUPUNGUZA MADHARA YANAYOTOKANA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA (HARM REDUCTION) 34

5.1 Utangulizi 34

5.2 Huduma ya Tiba Saidizi kwa Kutumia Dawa (MAT) 34

5.3 Huduma ya Kupunguza Madhara ya kuchangia Sindano kwa Watu Wanaojidunga (Needle and Syringe Program) 36

5.4 Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses) 37

5.5 Huduma za Kisaikolojia na Kijamii 38

5.6 Faida za Huduma za Tiba na Utengamao kwa Waraibu 39

5.7 Uwezeshaji wa Asasi 39

SURA YA SITA 40

USHIRIKIANO WA KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA 40

6.1 Utangulizi 40

6.2 Ushirikiano wa Kitaifa 40

6.3 Ushirikiano wa Kikanda 41

6.4 Ushirikiano wa Kimataifa 42

SURA YA SABA 44

CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA BAADAYE 44

7.1 Utangulizi 44

7.2 Changamoto 44

7.3 Mikakati 44

KIAMBATA NA. I 45

KIAMBATA NA. II 48

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 3.1: Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini kwa muongo mmoja (mwaka 2015 -2024) 10

Kielelezo na. 3.2 10

Kielelezo na. 3.3 11

Kielelezo Na. 3.4: Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi Waliokamatwa Kati ya Mwaka 2015-2024 11

Kielelezo na. 3.5: Mwenendo wa Idadi ya Watuhumiwa waliokamatwa 12

Kielelezo Na. 3.6: Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini Katika muongo mmoja (Mwaka 2015-2024).......................................13

Kielelezo na. 3.7 13

Kielelezo Na. 3.8: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa katika muongo mmoja (Mwaka 2015-2024) 14

Kielelezo Na. 3.9: 15

Kielelezo Na. 3.10: Kiasi cha Dawa nyingine za kulevya zilizokamatwa mwaka 2021- 2024 16

Kielelezo Na. 3.11: kiasi cha Methamphetamine, Skanka na MDPV kilichokamatwa kati ya Mwaka 2015 - 2024 17

Kielelezo Na. 3.12: 17

Kielelezo Na. 3.13: Kiasi cha Kemikali Bashirifu kilichoingizwa Nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2024 18

Kielelezo 3.14: Kiasi cha Kemika li Bashirifu zilizozuiliwa kuingia Nchini Mwaka 2017 hadi 2024..19

Kielelezo na. 3.15..19

Kielelezo Na. 3.16 Idadi ya kesi za dawa za kulevya zilizofunguliwa katika mahakama mbalimbali katika mwaka 2024 21

Kielelezo Na. 3.17: Ekari za Mashamba ya bangi zilizoharibiwa katika mikoa mbalimbali Nchini kwa Mwaka 2024.....................................23

Kielelezo namba.5.1: Idadi ya watu wenye uraibu waliosajiliwa kwenye vituo vya MAT kuanzia Mwaka 2017 hadi 2024......................................35

Kielelezo na 5.2: Idadi ya watu wenye uraibu waliosajiliwa katika Nyumba za Upataji Nafuu 2019-2024 nchini. 37

MAELEZO YA WAZIRI

Serikali imeendelea kupata mafanikio makubwa katika vita dhidi ya uzalishaji, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya nchini. Katika kipindi cha mwaka 2024, tumeshuhudia mafanikio makubwa yaliyopatikana kutokana na juhudi za Serikali ya awamu wa sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuweka rasilimali za kutosha katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Kwa upande wa dawa za kulevya za mashambani bangi imeongoza kukamatwa ikifuatiwa na mirungi. Serikali imefanikiwa kukamata shehena kubwa ya bangi kiasi cha tani 2,307.37 kati ya kiasi hicho, tani 2,303.2 ni bangi iliyozalishwa nchini na kiasi cha tani 4.17 ni bangi yenye kiwango cha juu cha kemikali ya THC, maarufu kama *Skanka* iliyoingizwa nchini kutokea baadhi ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Kiasi cha Skanka kilichokamatwa mwaka 2024, ni ongezeko la asilimia 89.8 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Hii inatokana na kuimarika kwa udhibiti wa biashara ya dawa za kulevya nchini. Mirungi ni dawa ya kulevya ya mashambani iliyofuatia kukamatwa, ambapo kwa mwaka 2024 kiasi cha tani 18.45 zilikamatwa katika operesheni mbalimbali nchini.

Dawa za kulevya zinazozalishwa viwandani zilikamatwa kiasi cha tani 1.7 za methamphetamine, kilogramu 433.02 za heroin na gramu 853 za cocaine. Haya ni mafanikio makubwa katika operesheni za kudhibiti usafirishaji wa dawa hizi kupitia bandari na mipaka ya nchi. Pia, kwa mara ya kwanza kilogramu tano za dawa ngeni ya kulevya aina ya methylene-dioxy-pyrovalerone (MDPV) zilikamatwa zikiingizwa nchini.

Pamoja na hayo, Serikali imeimarisha ufuatiliaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya ili zisichepushwe na kutumika kama mbadala au kutengeneza dawa za kulevya. Kwa mwaka 2024 kiasi cha kilogramu 19.2 na lita 22,682.4 za kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya kiasi cha kilogramu 56.78 na mililita 200 zilikamatwa. Aidha, serikali kupitia mifumo ya kielektroniki ilifanikiwa kuzuia uingizwaji wa tani 29.6 na lita 125 za kemikali bashirifu.

Serikali imeendelea kuratibu huduma za tiba ya Methadone kwa waraibu wa dawa za kulevya jamii ya afyuni hususani heroin ambapo huduma hiyo ilitolewa katika vituo 16 nchini ambavyo vimesajili waraibu 17,975. Kufanya usimamizi shirikishi kwa nyumba za upataji nafuu (sober houses) zipatazo 62 zilizohudumia waraibu 17,230 wa dawa mbalimbali za kulevya. Hatua hizi ni sehemu ya jitihada za Serikali kuhakikisha waraibu wanarejea kwenye jamii na kujenga maisha mapya yenye matumaini.

Natoa pongezi kwa wadau wote waliotoa mchango mkubwa katika mapambano haya wakiwemo vyombo vya ulinzi na usalama, wataalamu wa afya, wanaharakati na wananchi. Ushirikiano ni silaha kuu ya kushinda vita dhidi ya dawa za kulevya. Nawasihi wananchi wote kuendelea kuwa macho, kutoa taarifa na kushirikiana na Serikali ili kuifanya nchi yetu kuwa mahali salama na huru dhidi ya athari za dawa za kulevya. Pamoja, tunaweza!.

Mhe. William V. Lukuvi (Mb)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)

DIBAJI

Mapambano dhidi ya dawa za kulevya ni jukumu letu sote, na mafanikio yake yanahitaji mshikamano wa kitaifa na kimataifa. Kwa mujibu wa kifungu cha 60 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeendelea kutekeleza jukumu lake la kuandaa na kuwasilisha Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Bungeni kila mwaka. Taarifa hii ni nyenzo muhimu inayotoa tathmini ya kina kuhusu hali ya tatizo hili, juhudi zilizofanyika, changamoto, na hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa mustakabali wa Taifa letu.

Taarifa hii imegawanyika katika sura kuu saba. Sura ya kwanza inaelezea tatizo la dawa za kulevya duniani, sura ya pili inafafanua mikakati ya udhibiti wa dawa za kulevya na sura ya tatu inaelezea jitihada za udhibiti wa upatikanaji wa dawa za kulevya. Aidha, sura ya nne inaelezea juhudi za Mamlaka katika kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya, sura ya tano inafafanua jitihada za Mamlaka katika kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya. Sura ya sita inafafanua ushirikiano wa wadau katika udhibiti wa dawa za kulevya na taarifa hii inahitimishwa na sura ya saba ambayo imeainisha changamoto na mikakati ya kukabiliana nazo.

Mwisho, naomba nichukue fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira yake kubwa ya kutatua tatizo hili Nchini, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa miongozo yao sahihi juu ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya na Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), kwa uratibu na usimamizi wake mzuri juu ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya Nchini. Aidha, ninawashukuru wadau wote wa ndani na nje ya taasisi waliowasilisha taarifa muhimu zilizosaidia kufanikisha uandaaji wa taarifa hii. Ushirikiano wetu ndio msingi wa mafanikio katika vita dhidi ya dawa za kulevya.

Aretas J. Lyimo
KAMISHNA JENERALI
MAMLAKA YA KUDHIBITI NA
KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

FAHARASA

CCP	Chuo cha Polisi
DCEA	Drug Control and Enforcement Authority
DEA	Drug Enforcement Authority
DPP	Director of Public Prosecutions
GCLA	Government Chemist Laboratory Authority
MAT	Medically Assisted Therapy
MoU	Memorandum of Understanding
OSHA	Occupational Safety and Health Authority
PPP	Public Private Partnership
TB	Tuberculosis
TMDA	Tanzania Medicines and Medical Devices Authority
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
UNODC	United Nations Office on Drugs and Crime
UVIKO	Ugonjwa wa Virusi vya Korona
VVU	Virusi vya UKIMWI
ZDCEA	Drug Control and Enforcement Authority of Zanzibar

SURA YA KWANZA

HALI YA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI

1.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mwenendo wa hali ya tatizo la dawa za kulevya duniani kwa kutumia dondoo za Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2024 ambayo imeelezea biashara, matumizi, uzalishaji wa dawa za kulevya na matibabu kwa waraibu. Pia, sura hii inaelezea matumizi ya dawa za kulevya na jinsia, namna ukuaji wa sayansi na teknolojia ulivyoathiri matumizi na biashara ya dawa za kulevya, utoaji wa huduma kwa waraibu na udhibiti wa dawa za kulevya.

1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Duniani

Biashara na matumizi ya dawa za kulevya yamekuwa ya kishamiri duniani kwa miaka ya hivi karibuni. Moja ya sababu zilizochangia ongezeko la matumizi hayo ni kurejea kwa matumizi ya dawa aina ya vichangamshi (stimulants) kama vile cocaine na "ecstasy" baada ya kushuka kimatumizi na upatikanaji wakati wa janga la UVIKO 19. Taarifa ya hali ya dawa za kulevya duniani ya mwaka 2024 ilionesha kuwa mwaka 2022 takribani watu milioni 292 walitumia dawa za kulevya ikiwa ni ongezeko la asilimia 20 kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita.

Miongoni mwa dawa hizo ambazo kwa kipindi cha mwaka huo zimekuwa zikizalishwa na kutumiwa kwa wingi ni pamoja na bangi, heroin, metamphetamine, cocaine na ecstasy. Takwimu za mwaka 2022 zinaonesha kuwa takribani watu milioni 228 walitumia bangi, milioni 60 walitumia dawa za kulevya jamii ya afyuni, milioni 30 walitumia dawa jamii ya amphetamine, watu milioni 23.5 walitumia cocaine na "ecstasy" ilitumiwa na watu milioni 20. Wanaume wamekuwa watumiaji wakubwa wa cocaine na dawa jamii ya afyuni wakati wanawake wamekuwa wakitumia zaidi dawa tiba zenye asili ya kulevya kama Tramadol na Fentanyl.

Udhibiti wa Dawa mpya za kulevya (New Psychotropic Substances- NPS) ulifanikiwa kupunguza kiasi cha dawa hizo zilizoingizwa sokoni. Dawa hizo zilipungua kutoka aina 618 mwaka 2021 hadi aina 566 mwaka 2022.

Uwepo wa dawa za kulevya uliongeza matumizi, madhara na idadi ya watu waliopata matibabu ya uraibu. Madhara ya kiafya yaliyoripotiwa kwa watumiaji ni pamoja na magonjwa ya akili, maambukizi ya virusi vya UKIMWI na homa ya ini. Tafiti zinaonesha watu milioni 6.8 waliotumia dawa za kulevya walikuwa na maambukizi ya homa ya ini aina C, watu milioni 1.6 walikuwa na virusi vya UKIMWI na watu milioni 1.4 walikuwa na homa ya ini aina C pamoja na virusi vya UKIMWI.

Taarifa hiyo iliripoti kuwa vijana ni kundi lililo katika hatari ya matumizi ya dawa za kulevya za viwandani (synthetic drugs) kutokana na sababu kama vile, msukumo rika, upatikanaji rahisi wa dawa za viwandani, dhana potofu na uelewa finyu juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa hizo. Vijana hupata dawa hizi kupitia mitandao ya kijamii na wengine huletewa nyumbani. Katika kukabiliana na hali hii, jitihada kubwa zimeendelea kuchukuliwa ili kudhibiti uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na utoaji elimu na tiba kwa watu wenye uraibu.

1.2.1 Bangi

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya duniani ya mwaka 2024 ilionesha bangi imeendelea kutumika zaidi duniani ambapo takribani watu milioni 228 walitumia mwaka 2022. Idadi hiyo ni sawa na asilimia nne ya watu wote duniani ikiwa ni ongezeko la asilimia 28 katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Kwa mwaka 2022 Amerika ya Kaskazini imeendelea kuwa kinara wa matumizi ya bangi ambapo asilimia 19.8 ya watu kati ya miaka 15 na 64 waligundulika kutumia dawa hiyo.

Matumizi ya bangi miongoni mwa vijana bado ni tatizo katika maeneo mengi duniani. Nchini Canada matumizi ya bangi kwa vijana yameongezeka ambapo kumekuwa na ongezeko la uvutaji wa bangi kwa njia ya mvuke jambo ambalo limezua wasiwasi kuhusu hatari zinazotokana na matumizi ya dawa hizo hasa katika umri ambao matumizi ya dawa za kulevya yanaweza kusababisha madhara ya kudumu katika ukuaji wa ubongo. Hali hii inasababishwa na kuhalalishwa kwa matumizi ya bangi nchini humo.

Inakadiriwa kuwa mwaka 2019, asilimia 41 ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya yalitokana na matumizi ya bangi. Mwaka 2022, asilimia 49 ya nchi ziliripoti bangi kama dawa inayochangia sehemu kubwa ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya. Pia, asilimia 38 ya nchi ziliripoti kuwa bangi ni dawa iliyotumiwa na waraibu wengi walio kwenye tiba.

Afrika imeendelea kukua kwa kasi kwenye matumizi na biashara haramu ya bangi ambapo nchi za Afrika ya kaskazini zimeendelea kuwa kinara wa uzalishaji na usafirishaji wa bangi iliyosindikwa “hashish” kwenda nchi za Ulaya Magharibi. Aidha, taarifa zinaonesha kuwa watu wengi wanaotibiwa uraibu wa dawa za kulevya barani Afrika ni vijana wenye umri wa chini ya miaka 35.

1.2.1.1 Uhalalishaji wa Bangi na Athari zake

Maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kiafya na kisiasa ni miongoni mwa sababu zilizopelekea baadhi ya nchi duniani kuhalalisha kilimo na matumizi ya bangi. Nchi za Canada, Uruguay na majimbo 27 ya marekani yamepitisha sheria ya uzalishaji

na uuzaji wa bangi kwa matumizi yasiyo ya kitabibu. Nchi za uholanzi na Uswisi zinafanya utafiti ili kuelewa vyema athari za biashara na matumizi ya bangi isiyo ya kitabibu.

Tafiti zinaonesha kumekuwa na ongezeko la matumizi na idadi ya wanaopata matibabu kwenye nchi ambazo bangi imehalalishwa. Kwa mwaka 2021, kwenye Nchi za Ulaya takribani nusu ya watu waliopata huduma za matibabu ya uraibu wa dawa za kulevya kwa mara ya kwanza walikuwa wakitibiwa kwa matumizi ya bangi.

Barani Afrika uzalishaji na matumizi ya bangi yamekuwa yakiongezeka kwa kasi japo serikali za nchi hizo zimekuwa zikipambana kuepusha jamii na madhara yanayotokana na matumizi ya dawa hiyo.

1.2.2 Dawa za Kulevya Jamii ya Afyuni

Matumizi ya dawa za kulevya jamii ya Afyuni (opioids and opiates) yameendelea kutumika kwa kiasi kikubwa duniani. Kwa mujibu wa Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2024, watu takribani milioni 60 walitumia dawa hizo. Mwaka 2022, watu milioni 30 kati milioni 60 walitumia heroin sawa na asilimia 1.2 ya idadi ya watu wote duniani huku wanawake wakiwa ni asilimia 16 ya watumiaji wote.

Matumizi ya heroin yalipungua kwa kiasi kikubwa kutokana na kushuka kwa uzalishaji kwa asilimia 74 na kupungua kwa usambazaji duniani. Hali hii ilisababishwa na kupigwa marufuku uzalishaji wa dawa hiyo nchini Afghanistan hapo mwaka 2022. Myanmar imeibuka kuwa kinara wa uzalishaji wa heroin duniani kwa kuzalisha asilimia 54 ya dawa hiyo mwaka 2023. Aidha, Afghanistan, Iran, Uturuki na Nchi za Ulaya zilizo kwenye njia ya Balkan zimebaki kuwa njia kuu ya usafirishaji wa dawa hiyo.

Kupungua kwa uzalishaji wa heroin, kumesababisha ongezeko la matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya hasa Fentanyl na Tramadol kwenye nchi za Amerika ya Kaskazini, Afrika kaskazini na Magharibi na nchi za kusini mashariki mwa bara la Asia. Kwenye nchi za Amerika Kaskazini kumeripotiwa vifo vingi vilivyotokana na kuzidisha kiwango cha matumizi (overdose) ya dawa aina ya fentanyl tangu kipindi cha UVIKO mpaka 2022. Kwa ujumla theluthi mbili ya vifo duniani kote vitokanavyo na kuzidisha kiwango cha utumiaji (overdose) wa dawa za kulevya vinasababishwa na dawa jamii ya afyuni. Aidha, ukamataji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya umeongezeka katika maeneo mbali mbali duniani.

1.2.3 Hali ya Biashara na Matumizi ya Cocaine Duniani

Taarifa ya dawa za kulevya ya dunia kwa mwaka 2024 ilionesha biashara na matumizi ya dawa ya kulevya aina ya cocaine duniani yaliongezeka ambapo asilimia 0.45 ya idadi ya watu duniani ambao ni karibu sawa na watu milioni 23.5 walitumia cocaine mwaka 2022. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa cocaine ulifikia tani 2,757, ikiwa ni ongezeko la tani 453, sawa na asilimia 20, ikilinganishwa na mwaka 2021, ambapo uzalishaji ulikuwa tani 2,304.

Mabara ya Amerika pamoja na Nchi za Ulaya Magharibi na Kati yameendelea kuwa masoko makuu ya cocaine na kusambaa kwenye bara la Afrika na Asia. Hali hii ilisababishwa na kuongezeka kwa uhitaji wa dawa hiyo kwenye mabara hayo ndani ya miongo miwili iliyopita.

Miaka ya hivi karibuni kiwango cha usafirishaji wa cocaine kupitia mwambao wa bahari ya Atlantiki upande wa Afrika Magharibi kimeongezeka ambapo asilimia 80 ya shehena zilikamatwa. Kiwango hiki kiliongezeka hadi asilimia 86 mwaka 2022 na kufikia zaidi ya asilimia 90 mwaka 2023.

Aidha, matumizi ya cocaine yameendelea kuongezeka barani Afrika, hususan katika maeneo ya Afrika Magharibi na Kusini. Hali hii imedhihirika kupitia ongezeko la watu wanaopatiwa matibabu ya uraibu wa cocaine katika vituo vya afya. Katika nchi za Ulaya Magharibi na Kati, madhara yatokanayo na matumizi ya cocaine yanazidi kuonekana huku idadi ya waraibu wanaohitaji tiba ikiongezeka kwa kasi. Vilevile, matumizi makubwa ya cocaine yamechangia kuongezeka kwa vifo katika maeneo hayo.

Kwa ujumla, ongezeko la uzalishaji, usambazaji na matumizi ya cocaine linaendelea kuwa changamoto kubwa kwa jamii na mamlaka za udhibiti wa dawa za kulevya duniani, hususan katika kudhibiti athari zake kiafya na kijamii.

1.2.4. Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

Dawa hizi hutumika kwa madhumuni ya matibabu, lakini zinaweza kuwa na athari za uraibu ikiwa zitatumika kinyume na ushauri wa kitabibu. Taarifa ya dawa za kulevya duniani ya mwaka 2024 ilionesha kuwa, dawa tiba zenye asili ya kulevya zimeendelea kupungua kwenye matumizi ya kitabibu kutokana na kuchepushwa na kutumika kama dawa za kulevya. Uchepushaji wa dawa hizi kama Tramadol, Valium, Morphine, Pethidine na Fentanyl umeongezeka kwa kiasi kikubwa. Taarifa hiyo ilionesha kuwa takribani asilimia 87 ya watu waliokuwa wanasumbuliwa na maumivu makali waliokuwa wanahitaji dawa tiba zenye asili ya kulevya walikosa dawa hizi. Hii ni kutokana na uchepushwaji wa dawa hizo kwa matumizi yasiyo ya kimatibabu.

Afrika imeendelea kukumbwa na ongezeko la matumizi yasiyo ya kitabibu ya dawa tiba zenye asili ya kulevya. Kati ya mwaka 2018 na 2022, kulikuwa na ongezeko la asilimia 44 la matumizi hayo.

Kumekua na ongezeko la matumizi ya dawa hizo kwa wanawake hususani dawa za usingizi na zile za maumivu ili kukabiliana na matatizo ya msongo wa mawazo.

1.2.5 Dawa za Kulevya Jamii ya Amphetamine (Amphetanine Type stimulants - ATS)

Kundi hili linajumuisha dawa kama amphetamine, “methamphetamine” na “ecstasy” ambazo ni vichangamshi vinavyoathiri mfumo wa fahamu wa mtumiaji kwa kubadili jinsi ya kufikiri, kuhisi na kutenda. Kulingana na Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2024, inakadiriwa kuwa watu milioni 30 walitumia dawa hizi mwaka 2022, sawa na asilimia 0.6 ya idadi ya watu duniani.

Dawa hizi zimekuwa zikitumika zaidi katika maeneo ya Mashariki na Kusini-Mashariki mwa bara la Asia ikifuatiwa na Amerika Kaskazini. Inakadiriwa watu milioni 20 walitumia dawa ya aina ya “ecstasy” mwaka 2022, sawa na asilimia 0.4 ya idadi ya watu wote duniani.

Biashara ya dawa hizi, hasa methamphetamine, umeongezeka ambapo uzalishaji na usafirishaji wa dawa hiyo umefikia kiwango kikubwa kuwahi kushuhudiwa hapo kabla. Hali inadhihirishwa kwa uwepo wa masoko mapya ambayo yanaashiria ongezeko la matumizi ya methamphetamine katika maeneo mengi duniani.

1.2.6 Dawa Mpya za Kulevya (New Psychoactive Substances- NPS)

Hizi ni dawa za kulevya zinazozalishwa kwa kuiga kemikali zilizopo kwenye dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa kama vile bangi, mirungi, heroin na cocaine. Lengo likiwa ni kuficha uhalisia wake na kukwepa mkono wa sheria. Dawa hizi huwa na athari zaidi ya zile wanazoiga.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2024 ilionesha kupungua kwa dawa mpya za kulevya ambapo kwa mwaka 2022 uzalishaji wa dawa mpya za kulevya ulipungua kutoka aina 618 mwaka 2021 na kufikia aina 566, kati ya hizo aina 44 zilikuwa mpya kabisa. Kati ya mwaka 2020-2022, jumla ya nchi 52 Duniani ziliripoti kukamata dawa mpya, ikiwa ni ongezeko kutoka nchi 43 zilizoripoti kati ya mwaka 2010 hadi 2012. Taarifa hiyo ilionesha kuwa, watumiaji wengi wa NPS huzitumia bila kujua.

Kumekuwa na matumizi ya mchanganyiko wa dawa za kulevya (cock tail) inayojulikana kwa majina kama “Kush”, “Karkoubi” na “Gutter Water au Nyaope”, ambayo mara nyingi huwa na viambata mbalimbali vya dawa za kulevya na

dawa tiba zenye asili ya kulevya. Dawa za heroin, bangi, ketamine, MDMA, methamphetamine, cocaine, caffeine, codeine, morphine, valium, pombe, na viyeyushi (solvents) zimetajwa kutumika kutengeneza michanganyiko hiyo. Mchanganyiko huu unaweza kusababisha ulevi uliokithiri, uraibu wa haraka, madhara makubwa ya kiafya na katika baadhi ya matukio, vifo kutokana na kuzidisha kiasi.

1.3 Dawa za kulevya na jinsia (matumizi ya dawa za kulevya na wanawake)

Wanaume wameendelea kuongoza kwa matumizi ya dawa za kulevya Duniani ikilinganishwa na wanawake. Tafiti zinaonesha kwa kila watumiaji wanne wa dawa za kulevya mwanamke ni mmoja. Hata hivyo, uwiano huo hubadilika kulingana na aina ya dawa na maeneo ya kijiografia. Kwa mfano kwenye bara la Asia wanawake ni asilimia 9 ya watumiaji wote wa bangi tofauti na Amerika ya Kaskazini ambapo wanawake wanakadiriwa kufikia asilimia 45 ya watumiaji wote wa bangi.

Aidha, kwa upande wa dawa tiba zenye asili ya kulevya na vichangamshi jamii ya amphetamine (ATS) ripoti zinaonyesha wanawake wengi wamekuwa wakitumia dawa hizo kuliko wanaume na kwenye baadhi ya maeneo huwa sawa. Wanawake wanaotumia dawa hizi hujikuta wanapata madhara ya kiafya na kijamii hasa wale wanaojidunga ambapo maambukizi ya VVU na "hepatitis" yameongezeka.

Kumekuwa na mwitikio mdogo Afrika kwa wanawake wenye uraibu kujitokeza kupata tiba ambapo mwaka 2022 asilimia 10 tu ya wanawake wenye uraibu ndio waliohudhuria tiba ikiwa ni kiasi kidogo zaidi ya maeneo mengine Duniani. Hali hii inatokana uelewa mdogo walionao, unyanyapaa, kutopewa kipaumbele kwa vituo maalum ya kutibia wanawake na matatizo ya kiuchumi.

1.4 Dawa za kulevya na Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia

Ukuaji wa sayansi na teknolojia umeleta mabadiliko makubwa katika nyanja mbalimbali za maisha, zikiwemo afya, elimu, na mawasiliano. Hata hivyo, ukuaji wa sayansi na teknolojia umekuja na changamoto kubwa katika juhudi za kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya duniani. Taarifa ya Duniani ya 2024 ilionesha kuwa Teknolojia ya kisasa, kama vile mitandao ya siri (Dark Web) imekuwa ikitumika katika usambazaji wa dawa hizo.

Taarifa hiyo inaeleza kwamba mitandao ya kijamii imekuwa ikitumika kuhamasisha matumizi na biashara ya dawa za kulevya kupitia maudhui yake. Mitandao hiyo imekua ikieneza taarifa potofu kuhusu dawa za kulevya, ikiwemo kudai kuwa ni salama kutumia au kwamba zinasaidia kupunguza msongo wa mawazo taarifa ambazo si sahihi na kuchochea udadisi pamoja na kuanza matumizi ya dawa hizo.

SURA YA PILI

MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

2.1 Utangulizi

Tanzania inaendelea kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa kuzingatia Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya namba 5 ya mwaka 2015 pamoja na kufuata miongozo ya Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC). Serikali imeendelea kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa kuzingatia nguzo kuu nne ambazo ni; kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya (supply reduction), kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya (demand reduction), kupunguza madhara ya matumizi ya dawa za kulevya (harm reduction) na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa,kikanda na kimataifa (international cooperation). Sura hii inatoa taswira ya nguzo hizo ili kutoa mwongozo kwa sura zinazofuata.

2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction)

Lengo la nguzo hii ni kudhibiti uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini. Upatikanaji wa dawa za kulevya unahusisha kilimo, utengenezaji, uingizaji na usambazaji kupitia mipaka ya nchi kavu, majini na anga. Katika utekelezaji wa nguzo hii, mikakati ifuatayo huzingatiwa; Ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa kuhusu biashara ya dawa za kulevya, ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya, usimamiaji wa sheria ya dawa za kulevya nchini, udhibiti wa uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na kuratibu uteketezaji wa dawa za kulevya.

2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction)

Nguzo hii inazingatia utoaji wa elimu kama mkakati muhimu wa kuifanya jamii kujitambua na kujiepusha na matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini.

Katika utekelezaji wa nguzo hii Mamlaka inaratibu uelimishaji juu ya tatizo la dawa za kulevya katika jamii, ikiwa ni pamoja na kuandaa miongozo ya uelimishaji, kuwaandaa na kuwawezesha watoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya, kuratibu asasi zinazotoa elimu ya dawa za kulevya kwa umma, kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa klabu za dawa za kulevya na kuhuisha maudhui ya dawa za kulevya kwenye mitaala ya elimu.

2.4 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction)

Katika utekelezaji wa nguzo hii, utoaji wa huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya ni moja ya mkakati muhimu wa kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa hizo. Mraibu ni mgonjwa kama wagonjwa wengine, hivyo uraibu wa dawa za kulevya ni tatizo la kiafya na huathiri watumiaji na jamii. Tiba ya uraibu na magonjwa yanayoambatana ni muhimu ili kuwakinga watumiaji wa dawa za kulevya na jamii. Aidha, mikakati mingine ni kuratibu matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya, kuandaa miongozo ya matibabu, kufanya usimamizi shirikishi katika vituo vinavyotoa huduma za tiba na unasihi na kutoa elimu ya kupunguza madhara.

2.5 Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

Lengo la nguzo hii ni kuunganisha nguvu ya pamoja katika mapambano na udhibiti wa dawa za kulevya kitaifa, kikanda na kimataifa. Tatizo la dawa za kulevya ni suala mtambuka linalohusisha mitandao ya kihalifu iliyopo nchi mbalimbali duniani, hivyo mapambano dhidi ya tatizo hili yanahitaji ushirikiano na nguvu za pamoja kuanzia ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Katika utekelezaji wa nguzo hii, mikakati ifuatayo inazingatiwa; kubadilishana taarifa za kiintelejensia na uzoefu baina ya mataifa kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya, kutekeleza mikataba na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya, kuhudhuria mikutano na mafunzo kuhusu udhibiti wa dawa hizo, pamoja na kushirikisha wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi katika mapambano hayo.

SURA YA TATU

UDHIBITI WA UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA

3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza jitihada zilizofanyika katika kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya nchini kwa mwaka 2024. Jitihada hizi zilifanyika kwa ushirikiano na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama, Mahakama, Mamlaka za Udhibiti na wananchi.

3.2 Udhibiti wa Upatikanaji wa Dawa za Kulevya

Mwaka 2024, Mamlaka ikishirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi imefanikiwa kukamata dawa za kulevya za mashambani kama vile bangi na mirungi pamoja na dawa zilizozalishwa viwandani ambazo ni heroin, cocaine, methamphetamine, MDVP, mescaline, kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Mafanikio ya udhibiti huo yameainishwa kama ifuatavyo: -

3.2.1 Bangi

Mwaka 2024 kiasi cha tani 2,303.2 ambazo ni sawa na kilogram 2,303,195.86 za bangi zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa 7,981, kati yao wanaume 7,475 na wanawake 506**.** (***Kielelezo Na. 3.1 na Kielelezo Na.3.4).***

3.2.2 Mirungi

Kiasi cha tani 18.45 ambazo ni sawa na kilogram 18,449.75 za mirungi zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa 1,256 kati yao wanaume 1, 048 na wanawake 208**. (*Rejea Kielelezo Na.3.1 na Kielelezo Na.3.4).***

Kielelezo Na. 3.1: Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini kwa muongo mmoja (mwaka 2015 -2024)

Mwaka	Bangi (Tani)	Mirungi (Tani)
2015	22.01	16.60
2016	68.23	21.64
2017	52.19	67.81
2018	24.30	8.96
2019	21.51	9.07
2020	13.23	11.80
2021	22.74	10.93
2022	20.58	15.23
2023	1,757.56	202.74
2024	2,303.20	18.45

Chanzo: Kanzi data DCEA 2024

Kielelezo na. 3.2



Chanzo: Kanzi Data DCEA 2024

Kielelezo na. 3.3

	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021	2022	2023	2024
bangi	22.01	68.23	52.19	24.3	21.51	13.23	22.74	20.58	1757.56	2303.2
mirungi	16.6	21.64	67.81	8.96	9.07	11.8	10.93	15.23	202.74	18.45

Chanzo:Kanzi Data DCEA 2024

Takwimu katika vielelezo namba 3.1, 3.2 na 3.3 zinaonesha kuwa kiasi cha bangi kilichokamatwa kimeongezeka ukilinganisha na miaka iliyopita kutokana na kuongezeka kwa operesheni za ukamataji na uteketezaji wa mashamba ya bangi kutokana na taarifa kutoka kwa wananchi.

Kielelezo Na. 3.4: Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi Waliokamatwa Kati ya Mwaka 2015-2024

Mwaka	Watuhumiwa – Bangi	Watuhumiwa – Mirungi
2015	13,275	1,780
2016	17,889	2,397
2017	11,528	1,797
2018	9,744	1,185
2019	8,865	1,170
2020	7,601	1,156
2021	9,484	1,395
2022	10,277	1,491
2023	8,803	1,179
2024	7,981	1,256

Kielelezo na. 3.5: Mwenendo wa Idadi ya Watuhumiwa waliokamatwa



	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021	2022	2023	2024
Watuhumiwa wa Bangi	13,275	17,889	11,528	9,744	8,865	7,601	9,484	10,277	8,803	7,981
Watuhumiwa wa Mirungi	1,780	2,397	1,797	1,185	1,170	1,156	1,395	1,491	1,179	1,256

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2024

Kielelezo Na. 3.4 na 3.5 vinaonesha idadi ya watuhumiwa wa bangi na mirungi imeendelea kupungua ikilinganishwa na miaka iliyopita. Hali hii ni kutokana na juhudi kubwa zinazofanyika katika udhibiti. Vilevile, kupungua huko kumechangiwa na adhabu kali zinazotolewa pamoja na elimu inayoendelea kutolewa kuhusu dawa za kulevya.

3.2.3 Heroin

Jumla ya kilo 433.16 za heroin zilikamatwa nchini mwaka 2024 zikiwahusisha watuhumiwa 172, kati yao wanaume 151 na wanawake 21. (*Rejea kielelezo 3.4 Na. 3.6 na Kielelezo Na. 3.7)*.

3.2.4 Cocaine

Kiasi cha kilo 0.85 ambayo ni sawa na gramu 853 za cocaine zilikamatwa mwaka 2024 zikiwahusisha watuhumiwa 41 kati yao wanaume 40 na mwanamke 01. (*Rejea kielelezo 3.3)*.

Kielelezo Na. 3.6: Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini Katika muongo mmoja (Mwaka 2015-2024)

Mwaka	Kiasi cha Heroin kilichokamatwa (Kg)	Kiasi cha Cocaine kilichokamatwa (Kg)
2015	64.75	17.79
2016	42.26	18.52
2017	185.56	4.14
2018	16.94	7.67
2019	55.35	10.34
2020	349.81	4.52
2021	1,124.52	0.81
2022	254.71	1.73
2023	1,314.28	3.04
2024	433.16	0.85

Chanzo:Kanzi Data DCEA 2024

Kielelezo na. 3.7



Chanzo: Kanzi Data DCEA 2024

Takwimu zinaonesha kuwa kiasi cha heroin na cocaine kilichokamatwa kwa mwaka 2024 kilishuka ikilinganishwa na mwaka 2023. Hali hii inatokana kuzuiwa kwa kilimo cha mmea wa *Opium poppy* unaozalisha heroin nchini Afghanistan pamoja na kuimarika kwa jitihada za ukamataji na elimu kwa jamii. Kupungua kwa cocaine kumetokana na kusambaratishwa kwa mtandao wa biashara ya dawa hiyo.

Tani 1.4 za shehena ya bangi aina ya "skanka" iliyokamatwa mwezi Novemba 2024

Kielelezo Na. 3.8: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa katika muongo mmoja (Mwaka 2015-2024)

Mwaka	Heroin	Cocaine
2015	474	281
2016	716	263
2017	1,005	243
2018	463	148
2019	318	31
2020	428	80
2021	588	100
2022	409	122
2023	196	32
2024	172	41

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2024

Kielelezo Na. 3.9:



	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021	2022	2023	2024
Watuhumiwa wa Heroin	474	716	1,005	463	318	428	588	409	196	172
Watuhumiwa wa Cocaine	281	263	243	148	31	80	100	122	32	41

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2024

Takwimu zinaonesha kuwa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa na Heroin na Cocaine imeendelea kupungua kutokana na kushuka kwa biashara na matumizi ya dawa hizo pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa tatizo la dawa za kulevya kwa wananchi.

3.2.5 Dawa Nyingine za Kulevya

Katika miaka ya hivi karibuni kumeibuka uingizwaji na ukamataji wa dawa za kulevya ambazo ni ngeni hapa nchini. Dawa hizo zimeainishwa kama ifuatavyo;

3.2.5.1 Methamphetamine

Dawa hii ilikamatwa kwa mara ya kwanza mwaka 2021 ambapo kilo 430.77 zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa tisa (9). Mwaka 2023, ulikuwa ni mwaka wa kihistoria kwani kiasi cha tani 2.41 (Sawa na kilo 2,410.82) kilikamatwa kikiwa ni kiasi kikubwa zaidi cha dawa ya kulevya kuwahi kukamatwa kwa mkupuo tangu nchi yetu ipate uhuru. Aidha, methamphetamine iliendelea kukamatwa nchini ambapo mwaka 2024, ilikamatwa tani 1.73 ambayo ni sawa na kilo 1,729.2 ikihusisha watuhumiwa 23, wote wakiwa wanaume.

3.2.5.2 Bangi aina ya 'Skanka' na 'Hashish'

"Skanka" ni bangi chotara ambayo imetokana na bangi aina ya "*Cannabis sativa*" na "*Cannabis indica*" yenye kiasi kikubwa cha kemikali yenye sumu aina ya (tetrahydrocannabinol -THC) inayoingizwa nchini ikitokea nchi za kusini mwa Afrika. Aina hii ya bangi huchanganywa kwenye sigara na "shisha" kwa ajili ya

kuvutwa. Vilevile, huwekwa kwenye vyakula kama biskuti ‘*cookies*’, keki, jamu na juisi vinavyotengenezwa na wahalifu kwenye viwanda bubu kwa lengo la kukwepa mkono wa Sheria na kupata watumiaji wapya. Mwaka 2023, kilo 423.54 za skanka zilikamatwa. Mwaka uliofuatia tani 4.17 ambazo ni sawa na kilo 4,168.89 zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa 48 ikiwa wanaume 38 na wanawake 10.

Bangi iliyosindikwa ‘*Cannabis resin*’ maarufu kama ‘hashish’ au ‘charas’ ilikuwa ikikamatwa zaidi kwenye miaka ya tisini na mwanzoni mwa mwaka 2000. Baada ya hapo dawa hiyo haikukamatwa tena hadi mwaka 2024 ambapo kilo moja ya dawa hiyo ilikamatwa.

3.2.5.3. Mescaline

Dawa hii iliyo katika kundi la vileta njozi ‘hallucinogens’ hupatikana zaidi kwenye mabara ya Amerika ya Kaskazini na Kusini ikitokana na mmea jamii ya ‘cactus’. Mescaline inaweza kuwa kwenye mfumo wa vidonge, maji au unga. Kiasi cha gram 56.04 za dawa hii kilikamatwa kwa mara ya kwanza nchini mwaka 2022 ikimhusisha mtuhumiwa mmoja. Mwaka 2024 kwa mara nyingine kiasi cha gramu 560.8 sawa na nusu kilo ya dawa hiyo kilikamatwa.

3.2.5.4 Methylene-dioxy-pyrovalerone (MDPV)

MDPV ni dawa ngeni nchini, ikiwa katika kundi la vichangamshi na kutengenezwa kwa kutumia kemikali bashirifu pekee. Dawa hii imeongezwa nguvu ya kilevi inayozidi dawa nyingine za kundi hilo kama cocaine na methamphetamine, hivyo kuwa hatari zaidi kwa watumiaji. Mwaka 2024, kiasi cha kilo tano za dawa hiyo kilikamatwa kwa mara ya kwanza nchini kikimhusisha mtuhumiwa mmoja.

Kielelezo Na. 3.10: Kiasi cha Dawa nyingine za kulevya zilizokamatwa mwaka 2021- 2024

Na.	Mwaka	Methamphetamine (Kg)	Skanka (Kg)	Cannabis resin (Kg)	MDPV (Kg)	Mescaline (Gramu)
1	2021	430.77	-	-	-	-
2	2022	0.97	-	-	-	56
3	2023	2,410.82	426.60	-	-	-
4	2024	1,729.20	4,168.89	1.00	5	560.8

Kielelezo Na. 3.11: kiasi cha Methamphetamine, Skanka na MDPV kilichokamatwa kati ya Mwaka 2015 - 2024



	2021	2022	2023	2024
Methamphetamine	430.77	0.97	2,410.82	1,729.20
Skanka	0	0	423.54	4,168.89
MDPV	0	0	0	5

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2024

Kielelezo Na. 3.12:



	2021	2022	2023	2024
Watuhumiwa wa Methamphetamine	9	2	9	23
Watuhumiwa wa Skanka	0	0	0	48
Watuhumiwa wa MDPV	0	0	0	1

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2024

3.4 Kuzuia Uchepushwaji wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

3.4.1 Kemikali Bashirifu (Precursor Chemicals)

Kemikali bashirifu ni kemikali zinazotumika katika sekta mbalimbali za uzalishaji kutengeneza bidhaa za aina tofauti kama vile dawa tiba, nguo, uchenjuaji wa madini pamoja na matumizi ya nyumbani na shuleni. Hivyo, kemikali hizi hufanyiwa ufuatiliaji wa karibu ikiwemo ukaguzi katika maeneo ya bandari, bandari kavu, viwanja vya ndege na katika kampuni husika pamoja na kutoa elimu ya udhibiti kwa wadau wa kemikali ili kudhibiti kemikali zisichepushwe na kutumika kutengeneza dawa za kulevya.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mwaka 2024 kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Kampuni za kemikali 72 zimeingiza jumla ya tani 7,080.50 na lita 2,954,009.50 za Kemikali bashirifu kupitia maeneo mbalimbali ikiwemo bandari, viwanja vya ndege na vituo vya forodha vya mipakani kwa kuzingatia Sheria na taratibu za uingizaji wa kemikali nchini.

Kielelezo Na. 3.13: Kiasi cha Kemikali Bashirifu kilichoingizwa Nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2024

Mwaka	Kiasi cha Kemikali	
	Tani	Lita
2017	116,257.00	13,016,466.00
2018	1,534,064.00	11,247,555.00
2019	249,768.00	6,304,971.00
2020	96,062.44	4,256,161.00
2021	3,655.97	855,807.00
2022	11,389.00	5,711,266.00
2023	28,780.80	5,432,147.35
2024	7,080.50	2,954,009.50

Takwimu zinaonesha kwamba, katika kipindi cha mwaka 2024, uingizwaji wa kemikali bashirifu umepungua ikilinganishwa na mwaka 2022 na 2023, hali inayotokana na kupungua kwa mahitaji yake.

3.4.1.1 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu kupitia Mifumo ya Kielektroniki

Mamlaka imeendelea kufuatilia taarifa mbalimbali za usafirishaji haramu wa kemikali bashirifu kwenye mifumo ya kitaifa na kimataifa. Kwa kipindi cha Januari

hadi Disemba mwaka 2024, Mamlaka imezuia uingizwaji haramu nchini wa tani 29.6 na lita 125 za kemikali bashirifu kutokana na kukosekana kwa vibali vya uingizaji. Kemikali zilizozuiliwa ni Toluene, Acetone, Sulphuric acid, Ephedrine, Pseudoephedrine na Potassium Permanganate.

Kielelezo 3.14: Kiasi cha Kemika li Bashirifu zilizozuiliwa kuingia Nchini Mwaka 2017 hadi 2024

Mwaka	Kiasi (Tani)	Lita
2017	250.1	-
2018	23.1	-
2019	43.6	-
2020	57.6	-
2021	120.3	-
2022	98.3	85
2023	159.3	1,000
2024	29.6	125
Jumla	**781.9**	**1,210**

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2024

Kielelezo na. 3.15

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2024

Kiasi cha kemikali bashirifu kilichozuiliwa kwa mwaka 2024 kimepungua ukilinganisha na mwaka 2023 hali inayoonesha kuimarika kwa utii wa Sheria na taratibu zilizowekwa

3.5 Udhibiti wa Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

Dawa hizi hutumika kwa ajili ya matibabu ya binadamu na wanyama lakini zikitumika bila kufuata ushauri wa daktari huweza kusababisha uraibu. Udhibiti na usimamizi unafanywa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) chini ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura ya 219. Dawa hizi zisipodhibitiwa huweza kutumika kama dawa za kulevya kwa watu wa rika mbalimbali wakiwemo waraibu wa dawa za kulevya pale wanapokosa dawa walizozizoea. Katika Kudhibiti uchepushwaji wa dawa hizo Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya sura ya 95 inaharamisha biashara na matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya nje ya mfumo halali wa matibabu. Udhibiti wa uchepushwaji hufanyika kwa kufuatilia mienendo ya ungizaji wa dawa hizo, usambazaji wake na utunzaji wa kumbukumbu

Kwa mujibu wa taarifa ya TMDA ya mwaka 2024, jumla ya kilo 1,858.43 za dawa tiba zenye asili ya kulevya ziliingizwa nchini kutoka Nchi za Kenya, India na Afrika ya Kusini. Dawa hizi zimeingia kwa kufuata Sheria na taratibu kupitia vituo vya forodha vya mipakani na viwanja vya ndege.

3.6 Ukaguzi wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

Mamlaka imefanya kaguzi kwa lengo la kufuatilia mwenendo wa biashara, usambazaji na matumizi ya kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya katika maeneo 246 katika mikoa 10 ya Dar es Salaam, Mwanza, Songwe, Tanga, Mbeya, Arusha, Kigoma, Morogoro, Lindi na Mtwara.

Katika kaguzi hizo maeneo mbalimbali yamekaguliwa ikiwemo maduka 97 ya dawa tiba, hospitali na vituo vya afya 56, kampuni 52 za kemikali, vituo 24 vya forodha vya mipaka na vipenyo visivyo rasmi, kampuni nane za usafirishaji wa vifurushi, bandari kavu tano , bandari mbili na viwanda vya dawa tiba viwili.

Aidha, Kupitia kaguzi hizo Mamlaka imefanikiwa kukamata jumla ya lita 22,682.4 na kilo 19.2 za kemikali bashirifu, kilo 56.78 na mililita 200 za dawa za tiba zenye asili ya kulevya pamoja na watuhumiwa 20 walikamatwa na kuchukuliwa hatua kutokana na kutofuata taratibu za uingizaji na usafirishaji wa dawa na kemikali hizo.

3.7 Raia wa Kigeni waliokamatwa Nchini

Mwaka 2024, raia wa kigeni 11 walikamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na dawa za kulevya. Kati yao raia nane walitoka katika Nchi ya Pakistan, mmoja kutoka visiwa vya Commoro, mmoja kutoka Nchi ya Congo na mwingine kutoka Nchi ya Brazil, wote wakiwa ni wanaume.

3.8 Raia wa Tanzania waliokamatwa nje ya Nchi

Watanzania wameendelea kukamatwa wakijihusisha na dawa za kulevya wakiwa nje ya Nchi. Takwimu za mwaka 2024 zinaonesha jumla ya watanzania watano walikamatwa, ambapo kati yao wawili walikamatwa katika nchi ya Afrika Kusini, wawili nchini India na mmoja nchini Burundi, wote wakiwa ni wanaume.

3.9 Kesi za Dawa za Kulevya

Mapambano dhidi ya watu waliojihusisha na dawa za kulevya yamekuwa na mafanikio makubwa. Jumla ya mashauri 2,263 yakiwemo mashauri mapya 1,374 yalifunguliwa mahakamani mwaka 2024, mashauri 1,522 yalitolewa hukumu ambapo kati ya hayo Jamhuri ilishinda mashauri 1,201 sawa na asilimia 79.

Kielelezo Na. 3.16 Idadi ya kesi za dawa za kulevya zilizofunguliwa katika mahakama mbalimbali katika mwaka 2024

Kundi la dawa	Aina ya dawa	Idadi ya kesi zilizofunguliwa
Dawa za mashambani	Bangi	850
	Mirungi	340
Jumla		**1,190**
Dawa za viwandani	Heroin	137
	Cocaine	11
	Methamphetamine	33
	Methylene-dioxy-pyrovalerone (MDPV)	2
	Mescaline	1
Jumla		**184**
Jumla kuu		**1,374**

3.10 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya na Kemikali Bashirifu

Zoezi la uteketezaji hufanyika kwa mujibu wa sheria ili zisirudi kwenye matumizi na biashara haramu. Uteketezaji huo hufanyika chini ya usimamizi wa Hakimu au Jaji na hushuhudiwa na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Idara ya Usalama wa Taifa, Mkemia Mkuu wa Serikali, Baraza la Usimamizi wa Mazingira na waalikwa wengine ambao Kamishna Jenerali ataona inafaa kuwaalika.

Mwaka 2024, jumla ya kilo 614.12 za dawa za kulevya ziliteketezwa kwa amri ya mahakama katika kiwanda cha Saruji cha Twiga kilichopo eneo la Wazo mkoani Dar es Salaam. Kati ya hizo kilo 601.87 zilikuwa za methamphetamine na nyingine12.25 za heroin. Vilevile, lita 19,804.2 za kemikali bashirifu zilizokwisha

muda wake ziliteketezwa katika kiwanda ya Safewaste kilichopo wilaya ya Mkuranga, mkoa wa Pwani.

Methamphetamine kilo 602 na heroin kilo 13 zikiandaliwa kuchomwa kwenye kiwanda cha saruji cha Twiga kilichopo Wazo Hill jijini Dar es Salaam, mwezi Desemba 2024

Mamlaka ilifanikiwa kuteketeza dawa za kulevya aina ya bangi jumla ya kilogram 603.68 katika kiwanda cha saruji cha Dangote mkoani Mtwara.

Aidha, uteketezaji mwingine wa bangi ulifanyika kwa awamu mbili baada ya kesi kumalizika na mahakama kutoa amri ya utekekezaji. Awamu ya kwanza, tani 1.68 za bangi ziliteketezwa katika mji mdogo wa Chalinze mkoani Pwani na awamu nyingine kilogram saba za bangi ziliteketezwa wilayani Mkuranga, Pwani.

Operesheni dhidi ya kilimo cha bangi zilizofanyika katika mikoa mbalimbali nchini mwaka 2024, zilifanikisha uteketezaji wa jumla ya ekari 4,733 za mashamba hayo kama ilivyoainishwa katika jedwali lifuatalo:

Kielelezo Na. 3.17: Ekari za Mashamba ya bangi zilizoharibiwa katika mikoa mbalimbali Nchini kwa Mwaka 2024

Na.	Mkoa	Ekari
1.	Arusha	131
2.	Dodoma	14
3.	Iringa	04
4.	Katavi	03
5.	Lindi	35
6.	Mara	3,045
7.	Morogoro	1,165
8.	Mtwara	157
9.	Ruvuma	07
10.	Shinyanga	67
11.	Tabora	103
	Jumla	**4,733**

Bangi ikifyekwa bonde la mto Mara

3.11 Maboresho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Sura ya 95

Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya sura ya 95 imekuwa ikifanyiwa maboresho mara kwa mara ili kuondoa changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wake. Mwaka 2024 maboresho yalifanyika kwa kuhuisha Jedwali la Dawa za Kulevya na Kemikali Bashirifu kupitia Tangazo la Serikali Na.189 la tarehe 22, Machi, 2024. Maboresho hayo yalihusisha uingizaji wa aina mpya 59 za dawa za Kulevya na kemikali bashirifu tisa ambazo hazikuwepo kwenye sheria hii. Lengo la mabadiliko haya ni kudhibiti dawa za kulevya na kemikali bashirifu ambazo hazikuwa zinadhibitiwa hapa nchini.

SURA YA NNE

KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA (DEMAND REDUCTION)

4.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea juhudi za Mamlaka kwa kushirikiana na wadau katika kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya nchini. Mamlaka kwa kushirikiana na wadau imejikita katika kutoa elimu sahihi juu ya tatizo la dawa za kulevya ili jamii isijiingize katika matumizi ya dawa hizo. Elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya hutolewa kwa jamii kupitia vyombo vya habari, machapisho, semina, makongamano na maadhimisho mbalimbali ya kitaifa.

4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya

Dawa za kulevya ni moja kati ya changamoto zinazohatarisha afya, uchumi na usalama wa jamii kwa ujumla. Takwimu zinaonesha kuwa tatizo la matumizi ya dawa za kulevya limeongezeka kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni na linahusisha makundi mbalimbali ya kijamii ikiwa ni pamoja na vijana, wanawake na watoto. Dawa aina ya bangi imeendelea kuongoza katika matumizi ya dawa za kulevya nchini, hali hii imechangiwa na upatikanaji rahisi pamoja na ukuaji wa teknolojia. Dawa inayofuatia kwa matumizi ni heroin, mirungi, cocaine, dawa tiba zenye asili ya kulevya pia kumekuwa na viashiria vya matumizi ya methamphetamine (“chumvi, meth”).

Kutokana na ukuaji wa sayansi na teknolojia, kuadimika kwa dawa za kulevya zilizozoeleka na kuimarishwa kwa ulinzi na usalama katika maeneo mengi duniani kumeibuka kwa matumizi ya dawa mpya za kulevya. Dawa mpya za kulevya ni dawa zinazotengenezwa kwa kutumia kemikali bashirifu kuiga mfano wa dawa zilizopo ili kuficha uhalisia na kukwepa mkono wa sheria.

4.2.1 Matumizi ya Dawa za Kulevya kwenye Shisha

Shisha ni Nini?

Shisha ni kifaa kilichoungwa na mtungi wenye maji ambacho kwa asili hutumika kuvutia tumbaku kwa kutumia bomba au mrija. Pamoja na kwamba shisha ni kifaa lakini kuna dhana iliyojengeka katika jamii kwamba shisha ni mchanganyiko wa ladha mbalimbali zilizochanganywa na tumbaku. Miaka ya hivi karibuni Serikali imebaini uwepo ya dawa za kulevya na dawa tiba zenye asili ya kulevya zikichanganywa na tumbaku kwenye shisha. Majina mengine ya shisha ni pamoja na ‘*garimoshi*’ na *‘hookah’.*

Historia inaonesha kuwa matumizi ya shisha yalianza miaka mingi iliyopita katika jamii ya Kihindi na kusambaa katika maeneo mengine duniani. Tafiti mbalimbali zilizofanyika zimeonesha mchanganyiko wa shisha unaundwa na asilimia 30 ya Tumbaku na asilimia 70 ladha za matunda na vihifadhi maji. Ukuaji wa sayansi na teknolojia, umepelekea kuibuka kwa aina nyingine za shisha za kielektroniki maarufu kama "*e-cigarattes,shisha pens na vapes*".

Aina mbalimbali za shisha

4.2.2 Uchanganyaji wa Dawa haramu za Kulevya kwenye Shisha

Miaka ya hivi karibuni matumizi ya Shisha yamekuwa mlango wa kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya. Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa mwaka 2024 ilifanya uchunguzi wa matumizi ya dawa za kulevya kwenye shisha. Uchunguzi huo ulifanyika kwenye baadhi ya maeneo ya kumbi za starehe zilizopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Kigoma, Lindi, Mtwara na Morogoro.

Jumla ya sampuli 36 za shisha zilikusanywa kutoka kumbi za starehe katika mikoa hiyo na kubaini yafuatayo:

i. Sampuli nne zilibainika kuwa dawa za kulevya, sampuli moja ilikutwa na cocaine, moja ilikutwa na bangi, moja ilikutwa na fentanyl na sampuli nyingine ilikuwa na piperazine.

ii. Sampuli sita zilibainika kuwa na dawa tiba mbalimbali ikiwemo "*Paracetamol", "Phenacetin" na "Nifedipine".*

iii. Aidha, uchunguzi zaidi uliofanyika katika sampuli hizo za shisha umeweza

kubaini kuwa kiwango cha kemikali ya tumbaku aina ya nicotine kilikuwa kati ya asilimia 29 mpaka 70 kuliko kiwango cha kawaida cha kwenye sigara ambacho ni asilimia 0.5 hadi 2.

Matokeo ya uchunguzi huo yanaashiria kuwepo kwa tishio la madhara ya kiafya katika jamii inayotumia shisha kutokana na kuwepo kwa dawa za kulevya na kiwango kikubwa cha tumbaku kwenye shisha

Kukithiri kwa uchanganyaji wa dawa za kulevya pia ulidhihirika Zanzibar Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya (ZDCEA) ilikamata shisha za kielekroniki 300 zilizobainika kuwa na dawa za kulevya aina ya bufotenine iliyopo katika kundi la vileta njozi.

4.2.3 Sheria inasemaje kuhusu kuchanganya dawa za kulevya kwenye Shisha?

Serikali itaendelea na kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya kwa njia yoyote ikiwemo shisha. Kwa mujibu wa Sheria ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya ni kosa la jinai kumwekea mtu dawa za kulevya kwenye chakula, kinywaji au kitu chochote na kumfanya atumie dawa za kulevya bila kufahamu na pia ni kosa mtu kutumia dawa hizo kwa ridhaa yake. Vilevile, Sheria hiyo inakataza kumiliki vifaa kwa ajili ya matumizi ya dawa za kulevya na pia inakataza mmiliki au msimamizi yeyote wa nyumba, jengo, eneo au sehemu yoyote kuruhusu matumizi ya dawa za kulevya. Tahadhari inatolewa kwa wamiliki wote na wasimamizi wa maeneo ambayo shisha inatumika kuwa makini kuzuia matumizi ya dawa za kulevya.

4.3 Sababu zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya

Tatizo la matumizi ya dawa za kulevya limeendelea kuisumbua jamii hasa vijana. Hata hivyo, jitihada mbalimbali zimeendelea kufanyika ili kuiepusha jamii kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya. Sababu zinazochangia matumizi ya dawa za kulevya ni pamoja na: -

a. Msukumo rika au Kufuata Mkumbo

Vijana hujikuta wameingia katika matumizi ya dawa za kulevya kutokana na kujaribu kuendana na mitindo ya jamii, shinikizo, vishawishi kutoka kwa marafiki au watu wa rika moja ili aweze kutambulika au kuwa sehemu ya kikundi hicho.

b. Ukosefu wa Uelewa Sahihi Juu ya Madhara ya Dawa za Kulevya

Uelewa finyu juu ya madhara ya dawa hizo na kuona ni jambo la kawaida lisilo na madhara au hufikiria kwamba ni rahisi kudhibiti madhara yake, huchochea jamii kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya bila kujua hatari kubwa zinazoweza

kuwapata.

c. Urahisi wa Upatikanaji wa Dawa za Kulevya

Upatikanaji wa dawa za kulevya kwa urahisi huchangia watu wengi hasa wanaoishi katika mazingira magumu kujiingiza kwenye matumizi ya dawa hizo bila kujali madhara yanayoweza kuwapata baadaye. Bangi na mirungi zinaongoza kwa matumizi kwa sababu zimekuwa zikimea maeneo mengi nchini.

d. Ukuaji wa Sayansi na Teknolojia

Ukuaji huu umerahisisha uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya. Kwa upande wa uzalishaji teknolojia ya kisasa imewezesha uzalishaji kwa kiasi kikubwa na utengenezaji wa dawa mpya za kulevya. Usambazaji umerahisishwa zaidi baada ya kuibuka kwa mitandao ya kijamii ya wazi na siri "*dark web*", vifaa vya kisasa kama vile "*drones*" na sarafu ya kidijitali "*cryptocurrency*".

e. Migogoro ya Kifamilia

Wakati familia inapopitia mivutano, kutokuelewana au utengano huweza kupelekea baadhi ya wanafamilia kutumia dawa za kulevya wakiamini kuwa ni njia ya kukabiliana na matatizo yao na kupunguza maumivu wanayoyapitia kwa wakati huo bila kujali madhara yanayoweza kujitokeza.

f. Kushindwa Kutumia Stadi za Maisha

Kitendo cha mtu kukosa njia za kushughulikia changamoto zake za kila siku kutatua matatizo yanayomkabili, hujikuta anatumia njia zisizo sahihi kutafuta suluhisho ikiwemo matumizi ya dawa za kulevya.

g. Imani potofu

Hizi ni imani ambazo mara nyingi haziendani na ukweli, na husababisha watu kujihusisha na dawa za kulevya bila kuelewa hatari zinazohusiana nazo. Watu wengi wanaamini kwamba matumizi ya dawa za kulevya ni njia ya kushinda changamoto, kupata furaha au kujistarehesha.

h. Matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya bila kufuata ushauri wa daktari

Hizi ni dawa za hospitali zinazotumika kutibu magonjwa ya akili au kupunguza maumivu lakini zinapotumiwa bila ya kufuata ushauri wa daktari zinasababisha uraibu. Mfano wa dawa hizo ni Valium, Tramadol, Morphine, Pethidine na Fentanyl.

i. Magonjwa ya Akili

Magonjwa ya akili huchangia matumizi ya dawa za kulevya kwani wagonjwa wenye tatizo hilo hutumia dawa za kulevya kama njia ya kukabiliana na magonjwa hayo. Mfano wa magonjwa ya akili ni pamoja na saikosisi (kuchanganyikiwa), msongo

wa mawazo, sonona na kihoro.

j. Kurithi Vinasaba vya Uraibu wa Dawa za Kulevya

Vinasaba vina mchango mkubwa katika tabia na mwenendo wa mtu hivyo uwepo wa vinasaba vya uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya kwa mzazi mmoja huweza huchangia mtoto anayezaliwa kurithi uraibu huo.

4.4 Madhara ya Dawa za Kulevya

Matumizi na biashara ya dawa za kulevya yameendelea kuleta madhara katika nyanja mbalimbali kama vile afya, jamii, uchumi, mazingira na siasa. Madhara hayo yanaweza kuelezwa kama ifuatavyo:

4.4.1 Kiafya

Utumiaji wa dawa za kulevya huweza kusababisha matatizo ya kiafya ikiwemo magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza. Magonjwa yanayoambukiza ni pamoja na; kifua kikuu, VVU/ UKIMWI na homa ya ini (hepatitis B na C). Magonjwa yasiyoambukiza ni; shinikizo la damu, saratani, figo, moyo, kiharusi, uraibu ambao husababisha arosto kali pamoja na magonjwa ya akili. Aidha, matumizi hayo hupunguza uwezo wa kufikiri, kumbukumbu, maamuzi sahihi, kukosa usingizi, hamu ya kula kupungua, kuoza meno, na kudhoofika kwa kinga ya mwili na vifo vya ghafla.

Vilevile, waraibu wa dawa za kulevya wako kwenye hatari ya kupata matatizo ya mfumo wa uzazi kama vile ugumba, utasa na upungufu wa nguvu za kiume. Kwa wanawake, matumizi hayo yanaweza kusababisha kuvurugika kwa mzunguko wa hedhi, kuharibika kwa mimba, kuzaliwa kwa watoto wenye uraibu wa dawa, waliodumaa kimwili na kiakili, matatizo ya moyo, ulemavu na watoto njiti. Kwa ujumla, matumizi ya dawa za kulevya hupunguza muda wa kuishi kutokana na maradhi, uhalifu, au kuzidisha kiwango cha dawa.

4.4.2 Kijamii

Dawa za kulevya huchangia kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu kama vile; mauaji, wizi, ukahaba, utapeli, uporaji, uhalifu wa kimtandao na utekaji. Dawa hizo huathiri mahusiano ya kifamilia na kusababisha watoto kukosa malezi bora na ongezeko la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Jamii isiyotumia dawa za kulevya huweza kupata maambukizi ya VVU, homa ya ini, na kifua kikuu kutoka kwa waraibu wenye maradhi hayo. Pia, ajali zinazoweza kuepukika ni matokeo ya matumizi ya dawa za kulevya, zikiambatana na ulemavu, vifo, uharibifu wa mali na miundombinu. Kwa wanafunzi, matumizi ya dawa za

kulevya yanaathiri masomo yao kutokana na kupungua kwa kumbukumbu, utoro, utovu wa nidhamu na kuacha shule. Biashara ya dawa za kulevya huambatana na biashara nyingine haramu kama vile silaha, binadamu (kuwekwa bondi), ujangili na madanguro.

Aidha, Watumiaji wa dawa za kulevya hunyanyapaliwa kwenye jamii pamoja na familia zao. Wengine hufikia hatua ya kutengwa na kukosa huduma za afya, kukosa urithi na kusingiziwa makosa. Unyanyapaa huo huwafanya wale walioacha dawa za kulevya kushindwa kupata ajira na wakati mwingine kurudi kwenye matumizi ya dawa za kulevya (relapse) wakiamini watapata faraja.

4.4.3 Kiuchumi

Matumizi na biashara ya dawa za kulevya hudhoofisha nguvu kazi ya taifa. Serikali huingia gharama kubwa katika kufanya operesheni za kukamata wahalifu, kutoa tiba ya uraibu, kutoa elimu juu ya dawa za kulevya, kuendesha kesi mahakamani na kuhudumia wafungwa, badala ya kuelekeza rasilimali hizo kwenye maendeleo. Pia, biashara ya dawa za kulevya inachangia mfumuko wa bei, utakatishaji fedha, kuongezeka kwa tofauti ya kipato, umaskini na rushwa.

4.4.4 Kisiasa/Kidiplomasia

Biashara ya dawa za kulevya inaweza kusababisha machafuko ya kisiasa ikiwa ni pamoja na kuondoa serikali halali madarakani, kufadhili chaguzi na kuweka tawala zinazotetea maslahi ya wauzaji wa dawa za kulevya. Aidha, biashara hii kuchafua taswira ya Nchi kutokana na uwepo wa watanzania wanaokamatwa ughaibuni kwa kujihusisha na dawa hizo. Pia, kukithiri kwa biashara ya dawa za kulevya huathiri uwekezaji nchini.

4.4.5 Kimazingira

Matumizi ya dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga yanachangia uchafuzi wa mazingira pale sindano zilizotumika zinapotupwa hovyo kwenye maeneo kama viwanja vya michezo, fukwe na vituo vya daladala. Kilimo cha bangi na mirungi pia kinaharibu mazingira kwa kukata miti na kuharibu vyanzo vya maji. Moshi unaotokana na uvutaji wa dawa za kulevya unachafua hewa na kudhuru afya za watu waliopo karibu.

4.5 Jitihada zilizofanyika katika Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya

Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya unahusisha utoaji elimu kwa jamii ili isijiingize katika matumizi ya dawa hizo. "*Mwongozo wa Utoaji Elimu Juu ya Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini*" ulitumika kufikisha elimu sahihi kwenye makundi mbalimbali ya

kijamii. Kwa mwaka 2024 Mamlaka ilivunja rekodi ya utoaji elimu kwa kuwafikia watu takribani milioni 28 katika mikoa yote nchini. Mafanikio haya yamechagizwa na uwepo wa ofisi zake za kanda. Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wake ilitumia kila fursa iliyowezekana kufikisha elimu kwa makundi mbalimbali ya kijamii kupitia maadhimisho ya kimataifa, kitaifa, kikanda na kimkoa, mikutano, vyombo vya habari, semina, makongamano, matamasha na mafunzo kwa watoa elimu (Training of Trainers - ToT).

4.5.1 Kazi za Uelimishaji Zilizofanywa na Mamlaka

i. Siku ya Kupiga Vita Dawa za kulevya Duniani

Siku hii maalum ya kimataifa inaadhimishwa kila mwaka tarehe 26, Juni kwa lengo la kuikumbusha jamii kushiriki katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya. Mwaka 2024, maadhimisho hayo yalifanyika kitaifa jijini Mwanza tarehe 30, Juni katika uwanja wa Nyamagana. Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyewakilishwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika siku hiyo wadau wanaojihusisha na udhibiti wa dawa za kulevya walishiriki kuonesha kazi zao ikiwemo kutoa elimu kwa jamii.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, akizindua Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya wakati wa kilele cha Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani Jijini Mwanza, mwezi Juni 2024

ii. Elimu kwenye taasisi za elimu

Mamlaka ilitumia fursa ya ushirikiano na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ambayo ina klabu ya kupinga rushwa iliyoenea kwenye taasisi za elimu nchi nzima kutoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya. Kupitia ushirikiano huo wanafunzi wengi zaidi waliweza kufikiwa na elimu hiyo muhimu katika ngazi za shule ya msingi, sekondari vyuo vya kati na vyuo vikuu. Takribani

wanafunzi 500,000 walipata elimu hiyo.

iii. Walimu wa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo (Training of Trainers)

Mamlaka ilitumia fursa mbalimbali kuwafikia walimu hususan walimu wa malezi na walezi wa klabu za kupinga rushwa na dawa za kulevya kutoa elimu. Walimu walipitishwa kwenye Mwongozo wa utoaji elimu na kukabidhiwa nakala za rejea. Elimu ilitolewa kwa lengo la kufikisha elimu hiyo katika kutimiza majukumu yao ya kila siku. Takribani walimu 65 walijengewa uwezo juu ya tatizo la dawa za kulevya katika mikoa yote nchini.

iv. Mafunzo ya Uelimishaji kwa Walimu Zanzibar

Mamlaka (DCEA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar (ZDCEA) ilitoa elimu kwa washiriki 40 mjini Unguja ambao ni walimu walezi, Afisa Elimu wilaya, watumishi wa kituo cha tiba ya uraibu Kidimni, mwakilishi kutoka AMREF na watumishi wa ZDCEA

v. Maadhimisho na Matamasha

Maadhimisho ya kimataifa, kitaifa na kanda au ya kimkoa ambayo hukusanya watu wengi yamekuwa yakitumiwa na Mamlaka kufikisha elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya. Mamlaka ilishiriki maadhimisho mbalimbali ikiwemo: Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) Mkoani Dar es salaam, Maonesho ya Siku ya Wakulima (Nanenane), Uzinduzi wa Mbio za Mwenge mkoani Kilimanjaro, Maadhimisho ya Wiki ya Vijana inayoambatana na Kumbukizi ya Kifo cha Mwalimu Nyerere na Kilele cha Mbio za mwenge wa Uhuru mkoani Mwanza, Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani Songea mkoani Ruvuma na Maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Sheria jijini Dodoma.

Maadhimisho mengine ni Siku ya wanawake Duniani, Usalama Mahala pa Kazi (OSHA), Tamasha la Biti Titi Kibiti mkoani Pwani, Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, Kampeni ya *Familia yangu Haina Mhalifu* kwa kushirikiana na jeshi la polisi, Tamasha la utamaduni “*Bulabo”* mkoani Mwanza, Tamasha la Kitaifa la Kiutamaduni mkoani Ruvuma na Tamasha la wajasiriamali mkoani Kagera “*ijuka* “*Omuka.*

vi Vyombo vya Habari

Katika kuhakikisha jamii inapata uelewa juu ya tatizo la dawa za kulevya, Mamlaka ilitoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari ikiwemo runinga, redio, magazeti, radio za kijamii, tovuti, blogs na mitandao ya kijamii. Kupitia vyombo vya Habari, zaidi ya watu milioni 25 walifikiwa na elimu hiyo. Aidha, matangazo ya kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu tatizo la dawa za kulevya yalirushwa kupitia televisheni ya ITV kwa kipindi cha mwaka mzima.

Kamishna Jenerali, Aretas Lyimo, akishiriki kipindi kutoa elimu kwa jamii

Vii Elimu kwa wanahabari

Mwaka 2024 jumla ya wahariri 66 wa vyombo vya Habari walijengewa uwezo kulielewa tatizo la dawa za kulevya na kuchukua hatua stahiki. Mamlaka iliwajengea uwezo waandishi wa habari takribani 200 kutoka katika redio 12 za kijamii katika Kanda ya Pwani inayojumuisha mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma.

ix. Wadau wanaojihusisha na kemikali Bashirifu na Dawa Tiba Zenye Asili ya Kulevya

Mamlaka ilitoa mafunzo ya udhibiti wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya kwa wadau 783 wakiwemo wasimamizi wa kemikali, maafisa forodha, madereva, wajasiriamali wanaotumia kemikali na wamiliki wa maduka ya dawa katika mikoa ya Dodoma, Kigoma, Mtwara, Lindi, Tanga na Dar es salaam.

vi. Vyombo vya Ulinzi na Usalama

Elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya hutolewa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama ili kuwajengea uwezo katika kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya. Mwaka 2024, elimu hiyo ilitolewa kwa wanafunzi wa Chuo cha Raphael Kubaga, kilichopo Wilayani Mkinga, Mkoani Tanga, Maafisa wanafunzi wa chuo cha misitu mkoani Arusha, Chuo cha mafunzo ya Afisa Magereza kilichopo Kiwila Mkoani Mbeya, Chuo cha mafunzo ya polisi (CCP) mkoani Kilimanjaro na Maafisa magereza wanawake kutoka mikoa mbalimbali Tanzania iliyofanyika jijini Dodoma.

iv. Makundi mengine ya Kijamii

Katika kuhakikisha elimu ya dawa za kulevya inamfikia kila Mtanzania Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilitoa elimu kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, viongozi wa kimila, viongozi wa dini, chama cha Skauti, wafanyabiashara, wamiliki na Maafisa wasafirishaji, Akina mama wajawazito, wanavijiji ambako kilimo cha bangi kimekithiri, watoa huduma za Afya, Viongozi wa serikali za mitaa, wavuvi, waraibu wa dawa za kulevya na familia zao

4.5.2 Uelimishaji uliofanywa na Asasi za Kiraia

Katika lengo la kuifikia jamii Mamlaka hushirikiana na taasisi mbalimbali binafsi kufikisha elimu ya dawa za kulevya. Asasi zimeendelea kushirikiana na Mamlaka katika kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya kijamii, wakiwemo wanafunzi, wazazi na walezi, vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu na watu wenye uraibu. Jumla ya asasi 79 zilitoa elimu kwa wanufaika wapatao 4,143,955 kwa mwaka 2024. (***Rejea kiambata namba I).***

SURA YA TANO

KUPUNGUZA MADHARA YANAYOTOKANA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA (HARM REDUCTION)

5.1 Utangulizi

Dawa za kulevya zimeendelea kuwa tishio kubwa kwa afya ya jamii duniani kote. Kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya ni moja ya mikakati ya kukabiliana na matumizi ya dawa hizo katika jamii. Sura hii inaelezea jitihada zinazofanywa na serikali ikishirikiana na wadau katika kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya kwa waraibu. Miongoni mwa jitihada hizo ni kuanzisha na kuratibu huduma za tiba, utengamao, ushauri na unasihi katika vituo vya tiba saidizi kwa kutumia dawa (Medically Assisted Therapy-MAT), nyumba za upataji nafuu (sober houses), vitengo vya afya ya akili na Asasi za kiraia. Aidha waraibu wanaojidunga hupatiwa sindano ili kujidunga salama (Needle and Syringe Program-NSP)

5.2 Huduma ya Tiba Saidizi kwa Kutumia Dawa (MAT)

Matumizi ya dawa za kulevya, hasa zile za jamii ya afyuni kama heroin pamoja na dawa tiba zenye asili ya kulevya kama Tramadol, Pethidine, Morphine, Valium, Fentanyl na nyinginezo, yamesababisha madhara makubwa kwa jamii.

Dawa za Methadone na Suboxone (mchanganyiko wa Buprenorphine na Naloxone) hutolewa bure katika hospitali za serikali kwa watu wenye uraibu wa dawa jamii ya afyuni wanaopata huduma ya tiba katika vituo vya MAT chini ya uangalizi wa watoa huduma. Katika kuhakikisha kuwa huduma zinakuwa endelevu, baadhi ya watu wanaokidhi vigezo hupatiwa dawa za kutumia nyumbani kwa uangalizi wa familia (take-away dose). Lengo kuu la huduma ya kutumia dawa nyumbani ni kuwapunguzia safari za kufuata dawa kila siku waraibu wenye matatizo ya kijamii au mahitaji maalum, kama vile wajawazito, wafanyakazi, watu wenye ulemavu na wale wenye magonjwa ya kuambukiza. Utaratibu huo pia hupunguza msongamano wa waraibu katika vituo na kupunguza mzigo wa kazi kwa watoa huduma. Huduma ya MAT pia inajumuisha vipimo na matibabu ya magonjwa yanayoambatana na uraibu wa dawa za kulevya, kama kifua kikuu (TB), homa ya ini (Hepatitis B na C), na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Hadi kufikia Desemba 2024, huduma za MAT zilitolewa kwa waraibu 17,975 waliosajiliwa, ambapo kati yao, 17,208 walikuwa wanaume na 767 wanawake. Takwimu zinaonesha kwamba idadi ya waraibu wapya wanaosajiliwa imepungua

kutoka 2,219 mwaka 2023 hadi 2,060 mwaka 2024. Hali hii inaashiria kuongezeka kwa udhibiti wa upatikanaji na uhitaji wa dawa za kulevya unaofanywa na Serikali.

Kielelezo namba.5.1: Idadi ya watu wenye uraibu waliosajiliwa kwenye vituo vya MAT kuanzia Mwaka 2017 hadi 2024

Na	Jina la Kituo	Wanaume	Wanawake	Jumla	Mkoa
1.	MAT Hospitali ya Taifa ya Muhimbili	3,764	152	3,916	Dar es Salaam
2.	MAT Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala	3,717	258	3,975	
3.	MAT Hospitali ya Rufaa ya Temeke	3,405	105	3,510	
4.	Kituo Kidogo Gereza la Segerea	627	63	690	
5.	Kituo Kidogo Round Table-Mbagala				
6.	Kituo Kidogo kwenye Kituo cha Afya Tegeta				
7.	Kituo Kidogo kwenye Hospitali ya Wilaya ya Vijibweni-Kigamboni				
8.	MAT Hospitali ya Rufaa ya Wilaya, Tumbi Kibaha	553	06	559	Pwani
9.	MAT Hospitali ya Wilaya, Bagamoyo	799	13	812	
10.	MAT Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya	535	19	554	Mbeya
11.	MAT Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekou Toure	787	40	827	Mwanza
12.	MAT Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mount Meru	706	40	746	Arusha
13.	MAT Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Bombo	1,196	33	1,229	Tanga
14.	MAT Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Afya ya Akili, Itega	606	23	629	Dodoma
15.	MAT Kituo cha Afya Tunduma	196	6	202	Songwe
16.	MAT Gereza la Kihonda	317	9	326	Morogoro
	Jumla	**17,208**	**767**	**17,975**	

Aidha, Mamlaka imefanikiwa kuongeza vituo vidogo viwili (Satellite clinic) vya MAT katika wilaya za Muheza Tanga na Chalinze Pwani. Vituo hivyo vimekwisha jengwa na viko katika hatua ya uwekaji samani (Furnishing stage) tayari kwa kuanza kutoa huduma. Vile vile, Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Dunia (Global Fund)

iko kwenye ujenzi wa vituo vitatu vya MAT vinavyopatikana Moshi-Kilimanjaro, Kahama-Shinyanga na kituo kidogo (Satellite Clinic) kilicho Mkuranga-Pwani.

Waraibu wanaohudumiwa katika vituo vya MAT, huibuliwa kutoka mitaani na kuandaliwa katika ngazi ya jamii kwa kuwapatia huduma ya unasihi kabla ya kufikishwa katika vituo vya tiba. Kazi ya kuwaandaa waraibu hufanywa na asasi za kiraia zenye uzoefu na tatizo hilo ambazo huwapa elimu ya madhara ya dawa za kulevya, namna bora ya kuachana nazo na huduma za tiba zinazopatikana katika vituo vya MAT na kuwapeleka katika vituo husika kwa hatua ya usajili na kuanza huduma ya tiba. Zifuatazo ni asasi za kiraia zilizowaibua waraibu kutoka mitaani;

Orodha ya asasi za kiraia zilizoibua waraibu kwa mwaka 2024

1. Community Peers for Health and Environment Organization (CPHEO)
2. Tandika Youth Rehabilitation Handcraft Group (TAYOHAG)
3. Tanzania Network for People Who Use Drugs (TANPUD)
4. Organisation of Youth Against Risk Behaviours (OYARB)
5. Gift of Hope Foundation
6. Drug Abuse and Recovery Organization (DARO)
7. Foundation for Legal and Health Support (FLHS)
8. Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA)
9. Kimara Peer Educators and Health Promotors
10. Mapambano ya UKIMWI na Kifua Kikuu Temeke (MUKIKUTE)
11. Youth Volunteers Against Risk Behaviors (YOVARIBE)
12. Youth and Community Rehabilitation (YCR)
13. Peer to Peer Supporting Group
14. Steps Tanzania
15. Kibao Salama Foundation

5.3 Huduma ya Kupunguza Madhara ya kuchangia Sindano kwa Watu Wanaojidunga (Needle and Syringe Program)

Huduma za kupunguza madhara kwa waraibu wanaotumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga zinatolewa katika Asasi maalum za kiraia, ambapo waraibu wanapewa sindano ili kujidunga salama. Huduma hizi zinawawezesha wajidunga kupunguza hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa yanayosambazwa kupitia damu, kama vile VVU/UKIMWI, Homa ya Ini aina B na C na magonjwa ya ngono. Zifuatazo ni asasi za kiraia zilizohudumia waraibu wajidunga;

Asasi zilizotoa huduma hizi ni;-

1. Organisation of Youth Against Risk Behaviours (OYARB)
2. Gift of Hope Foundation
3. Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA)

4. Kimara Peer Educators and Health Promotors
5. Mapambano ya UKIMWI na Kifua Kikuu Temeke (MUKIKUTE)
6. Youth Volunteers Against Risk Behaviors (YOVARIBE)
7. Youth and Community Rehabilitation (YCR)
8. Peer to Peer Supporting Group
9. Kibao Salama Foundation

5.4 Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses)

Huduma za tiba na utengamao hutolewa kwa njia mbalimbali na moja ya njia hizo ni kupitia huduma za Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses) ambapo watumiaji wa dawa za kulevya na vilevi vingine hupatiwa huduma kwa kipindi cha miezi minne au zaidi ili kuwaondoa katika utegemezi wa dawa hizi kwa kutumia hatua 12 za upataji nafuu. Huduma zinazotolewa ni za kisaikolojia na kijamii pamoja na tiba kwa njia ya mazoezi na kazi kwa kutumia wataalamu wa ndani au nje ya nyumba. Nyumba hizi huendeshwa na Asasi za kiraia au watu binafsi kwa kufuata Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu wa Tanzania bara ambao unasimamiwa na Mamlaka.

Kuanzia mwaka 2019 hadi kufikia Disemba 2024 jumla ya watu 18,944 wenye uraibu walihudumiwa katika nyumba za upataji nafuu. Mwaka 2024 jumla ya watu 3,307 wenye uraibu walihudumiwa ambapo wanaume walikuwa 3,042 na wanawake 265 (rejea jedwali na. 5.4 na Kiambata II)

Kielelezo na 5.2: Idadi ya watu wenye uraibu waliosajiliwa katika Nyumba za Upataji Nafuu 2019-2024 nchini.

Mwaka		**2019**	**2020**	**2021**	**2022**	**2023**	**2024**	**Jumla**
Idadi	Me	3,609	2,103	2,949	3,056	3,283	3,042	**18,042**
	Ke	74	74	160	124	205	265	902
Jumla		**3,683**	**2,177**	**3,109**	**3,180**	**3,488**	**3,307**	**18,944**



Ramani inayoonesha mikoa yenye nyumba za upataji nafuu kwa Tanzania bara

5.5 Huduma za Kisaikolojia na Kijamii

Hii ni huduma endelevu inayolenga kukidhi mahitaji ya mtu kimwili, kihisia, kijamii, kiroho na kiakili. Aidha, changamoto za kisaikolojia na kijamii zimechangia kuingiza watu kwenye uraibu wa dawa za kulevya, Taasisi za serikali, Asasi za kiraia na Mashirika ya kimataifa yamekuwa yakitoa huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa watumiaji wa dawa za kulevya na jamii yake kama ndugu, jamaa na marafiki wa karibu. Huduma zitolewazo ni unasihi kwa waraibu, tiba za mabadiliko ya kitabia, huduma za msaada wa kwanza wa kisaikolojia, unasihi kwa familia, tiba na tathmini za afya ya akili na kuunganisha familia. Hivyo, huduma hizi zimeendelea kuwa sehemu ya tiba ya uraibu wa dawa za kulevya kwa kuwa zinashughulika na kiini cha tatizo lililomfanya mtu kuingia kwenye uraibu.

5.6 Faida za Huduma za Tiba na Utengamao kwa Waraibu

Huduma za tiba na utengamao zina faida zifuatazo katika kudhibiti tatizo la dawa za kulevya:

i. Kukuza uchumi wa nchi na kurejesha nguvukazi kutokana na kuimarika kiafya na kutumia stadi za kazi zinazowapa fursa ya kujiajiri na kuajiriwa.
ii. Kupunguza matumizi na biashara ya dawa za kulevya na uchepushwaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya.
iii. Kupunguza matendo ya uhalifu na uvunjaji amani katika jamii
iv. Kutoa fursa kwa watu wenye uraibu kupata tiba ya uraibu na magonjwa yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya
v. Kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI, kifua kikuu na homa ya ini
vi. Kuondoa unyanyapaa katika jamii kwa waraibu wa dawa za kulevya
vii. Kupunguza vifo vinavyotokana na maradhi, uhalifu, kuzidisha kiasi cha matumizi ya dawa na magonjwa yasiyoambukiza
viii. Kuwarejesha watu waliokuwa na uraibu kwenye familia zao.

5.7 Uwezeshaji wa Asasi

Serikali kupitia Mamlaka ina wajibu wa kuratibu na kuziwezesha asasi mbalimbali zinazofanya kazi ya kudhibiti tatizo la dawa za kulevya nchini kama vile utoaji elimu kwa jamii na upunguzaji madhara ya matumizi ya dawa hizo. Katika kutekeleza jukumu hilo Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ikishirikiana na wadau imewezesha asasi kifedha, mafunzo, miongozo na vifaa. Asasi zifuatazo ziliwezeshwa kifedha;

Asasi zilizowezeshwa kifedha katika mwaka 2024;
1. Youth Volunteers Against Risk Behaviors (YOVARIBE)
2. Youth and Community Rehabilitation (YCR)
3. Gift of Hope Foundation
4. Organisation of Youth Against Risk Behaviours (OYARB)
5. Peer to Peer Supporting Group
6. Foundation for Legal and Health Support (FLHS)
7. Drug Abuse and Recovery Organization (DARO)
8. Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA)
9. Tanzania Social Foundation for a Drug Free Generation (TSFDG)
10. Kimara Peer Educators and Health Promotors
11. Steps Tanzania
12. Mapambano ya Ukimwi na Kifua Kikuu Temeke (MUKIKUTE)
13. Kibao Salama Foundation
14. Nurget Development in Tanzania
15. Empowercare Foundation

SURA YA SITA

USHIRIKIANO WA KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA

6.1 Utangulizi

Tatizo la dawa za kulevya ni uhalifu wa kupangwa unaovuka mipaka hivyo linahitaji jitihada za pamoja kulikabili kuanzia ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika mwaka 2024, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya imeendelea kutekeleza mkakati huu kwa kuendeleza ushirikiano na wadau kama ilivyofafanuliwa;

6.2 Ushirikiano wa Kitaifa

Jitihada zilizofanyika katika kudhibiti dawa za kulevya nchini zilizoainishwa kwenye sura ya tatu hadi sura ya tano ni matokeo ya ushirikiano wa Mamlaka na wadau wa ndani kutoka serikalini na taasisi binafsi. Ushirikiano huo uliwezesha ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya, kuteketeza dawa za kulevya, utoaji elimu, kutoa tiba ya uraibu wa dawa za kulevya, kuendesha kesi mahakamani, kupima sampuli za dawa za kulevya, kutunza wahalifu wa dawa za kulevya, kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya, nk. Hata hivyo, kuna baadhi ya shughuli zilizotekelezwa kwa ushirikiano na wadau wa ndani ya nchi ambazo hazikuzungumziwa kwenye sura zilizotajwa, ikiwemo:-

i. Kukamilisha Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa ushirikiao na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)

ii. Kusaini makubaliano (MoU) na maduka 35 ya dawa tiba na kampuni 11 za kemikali ili kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya kupitia mradi wa ushirikishwaji wa Sekta Binafsi (PPP) .

iii. Mamlaka iliwajengea uwezo Kamati ya Kudhibiti Dawa za Kulevya kutoka Baraza la Wawakilishi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar (ZDCEA) na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Zanzibar kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya.

iv. Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali iliwajengea uwezo maafisa wa DCEA kuhusu uchunguzi wa kikemia wa sampuli za dawa za kulevya.

v. Mamlaka ilishiriki kikao cha wadau wa Usalama wa Usafiri wa Anga (*Aviation Security*) kujadili uanzishaji wa Mfumo wa Utunzaji wa Taarifa za Wasafiri (*Passenger Informations & Passenger Names Record System*)

Makamishna Jenerali wa DCEA na ZDCEA wakionesha Hati za Makubaliano (MoU) walizosaini ili kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya Nchini

6.3 Ushirikiano wa Kikanda

Mamlaka imeendelea kuimarisha uhusiano wa kikanda na mataifa mbalimbali katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya kwa kubadilishana taarifa za kiintelijensia, kubadilishana uzoefu wa mapambano ya dawa za kulevya, kuimarisha usalama wa mipaka pamoja na utambuzi wa mbinu mbalimbali zinazotumika kuficha na kusafirisha dawa za kulevya. Ushirikiano huo ulikuwa katika nyanja zifuatazo:

i. Mamlaka ilishiriki mkutano ulioratibiwa na Taasisi ya Kudhibiti Dawa za Kulevya ya Marekani (DEA-*African Division)* kuhusu uchepushwaji wa kemikali bashirifu katika utengenezaji wa dawa za kulevya.
ii. Mamlaka imeshiriki Mkutano wa Kwanza wa Mawaziri wa Ukanda wa Magharibi ya Bahari ya Hindi kuhusu udhibiti wa usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya ulioandaliwa na UNODC
iii. Mamlaka imeshiriki kikao cha kujadili namna ya kukabiliana na uhalifu unaofanyika kupitia njia ya Kusini (*Southern Route Partnership Conference*)
iv. Mamlaka imeshiriki kikao cha Wataalam wa Nchi zinazounda *Trilateral Planning Cell* (TPC) kujadili masuala mbalimbali yanazohusu mapambano dhidi ya dawa za kulevya.
v. Mamlaka imeshiriki mkutano wa kwa njia ya mtandao (*Global Coalition Against Synthetic Drugs*) uliolenga kuimarisha mbinu za kudhibiti dawa za kulevya za viwandani na dawa mpya za kulevya.

vi. Mamlaka imeshiriki warsha ya uchunguzi wa kikemia kwa kutumia vifaa vya uchunguzi vinavyotumia mbinu za kisasa za utambuzi (*Mass Spectrometry & Chromatography*) iliyoandaliwa na kampuni ya *Africa Biosystem Limited*.

vii. Mamlaka imeshiriki mafunzo udhibiti wa kemikali bashirifu na uchunguzi wa kikemia yaliyoratibiwa na Shirika la Kudhibiti Silaha za Kemikali (*Organisation for Prohibition of Chemical Weapons* – OPCW).

viii. Mamlaka ilibadilishana uzoefu na Tume ya Kupambana na Dawa za Kulevya ya nchini Zambia (*Drug Enforcement Commission* - DEC) juu ya ukamataji na uelimishaji.

ix. Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania Bara (DCEA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar (ZDCEA) ziliandaa Mkutano wa Tatu wa Sekretarieti ya Tume ya Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Nchi zilizo Mashariki na Kusini mwa Afrika (*Eastern and Southern Africa Commission on Drugs* – ESACD)

x. Mamlaka imeshiriki mkutano ulioratibiwa na UNODC Nairobi, Kenya kwa lengo la kupitia na kujadiliana juu ya rasimu ya ripoti ya kikanda kuhusu Dawa za Kulevya za kutengenezwa katika Nchi za Ukanda wa Afrika Mashiriki.

Wajumbe wa mkutano kati ya Tanzania na Zambia kuhusu masuala ya ulinzi uliofanyika Nchini Zambia

6.4 Ushirikiano wa Kimataifa

Mamlaka imendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa katika kudhibiti dawa za kulevya, kupunguza uhitaji na madhara yanayotokana na dawa hizo. Katika kuimarisha ushirikiano na taasisi za kimataifa, mamlaka imetekeleza majukumu yafuatayo:

i. Mamlaka ilishiriki mkutano ulioratibiwa na Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Duniani (*The Commission on Narcotic Drugs* - CND) na Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (*The International Narcotics Control Board* - INCB)

uliolenga kutambua changamoto mbalimbali pamoja na mipango madhubuti inayofanywa na Nchi Wanachama wa INCB katika kudhibiti uzalishaji wa dawa za kulevya.

ii. Mamlaka imeshiriki mafunzo kuhusu kudhibiti usafirishaji wa dawa kulevya na makosa yatokanayo na dawa za kulevya (*Counteracting Drug Trafficking and Related Crimes*).

iii. Mamlaka ilishiriki mafunzo ya Kimataifa kuhusiana na Haki za Binadamu (*International Humanitarian Law & Human Rights Seminar*)

iv. Mamlaka ilijengewa uwezo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Kimataifa wa Kufuatilia Uchepushwaji wa Kemikali Bashirifu (*Pre-Incident Communication System*) zinazotumika kutengeneza dawa za kulevya yaliyotolewa na Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (*International Narcotic Control Board* – INCB).

v. Mamlaka imeshiriki mafunzo maalumu ya Mtaala wa Kimataifa wa Kinga kwenye dawa za kulevya (*Universal Prevention Curriculum* – UPC) kutoka Shirika la Kimataifa la Colombo Plan. Mafunzo haya yalijikita katika kuwajengea uwezo watumishi katika kutoa huduma bora za kinga kwenye jamii kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.

vi. Mamlaka imeshiriki mafunzo ya utayari na kujilinda wakati operesheni pamoja na dharura *Personal Recovery* yaliyolenga kuwajenga uwezo maafisa wa vyombo vya ulinzi na usalama kupambana na wahalifu pamoja na hali za hatari na dharura wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Mafunzo haya yaliratibiwa na Shirika la Kupambana na Dawa za Kulevya la Nchini Marekani (*Drug Enforcement Authority* – DEA).

SURA YA SABA

CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA BAADAYE

7.1 Utangulizi.

Katika utekelezaji wa mikakati ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya mwaka 2024, Mamlaka ilipata mafanikio ambayo yametokana na uwezeshaji uliofanywa na Serikali, ushirikiano na Vyombo vya Ulinzi na Usalama, wadau na wananchi pamoja na uweledi wa maafisa wa Mamlaka katika kudhibiti na kupambana na dawa hizo. Licha ya kupata mafanikio hayo zipo changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu hayo na mikakati iliyowekwa kukabiliana nazo. Changamoto na mikakati hiyo imeainishwa kama ifuatavyo:-

7.2 Changamoto

1. Uelewa mdogo wa jamii juu ya tatizo la dawa za kulevya,
2. Ukuaji wa kasi wa sayansi na teknolojia,
3. Kukinzana kwa sheria ya kudhibiti na kupamabana na dawa za kulevya katika Nchi nyingine,
4. Jiografia ya Nchi ikihusisha milima na maeneo zinapolimwa dawa za kulevya aina ya bangi na mirungi, Pamoja na vipenyo vingi vya bahari na nchi kavu visivyofikika kwa urahisi.
5. Unyanyapaa kwa waraibu unarudisha nyuma juhudi za Mamlaka kudhibiti tatizo la dawa za kulevya.

7.3 Mikakati

1. Kuongeza juhudi na wigo mpana wa utoaji wa elimu hasa kwa maeneo ya vijijini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.
2. Kuendelea kuimarisha ushirikiano na Mamlaka nyingine za udhibiti wa dawa za kulevya ndani na nje ya nchi pamoja na kuwashirikisha wadau wote kwa ujumla.
3. Kuendelea kuboresha sheria ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya kulingana na mahitaji.
4. Kuendelea kushirikiana na wadau kuongeza huduma za tiba na utengamao katika maeneo yenye uhitaji.
5. Mafunzo kwa watendaji katika udhibiti wa dawa za kulevya ili kuendana na kasi ya ukuaji wa sayansi na teknolojia.

Kiambata Na. I

Orodha ya Asasi za Kiraia zilizofanya Kazi za Utoaji Elimu kwa Mwaka 2024

1. Action Plan Organization
2. Akili Platform Tanzania
3. Alliance for Youth Advancement (AFYA)
4. Alpha Visible Community Development
5. Amani Sports Academy
6. Anti Alcoholism and Drug Addiction Organization (AADAO)
7. Bahibo Mental Health Organization (BMHO)
8. Beacon Teens Challenge
9. Blue Cross Society of Tanzania
10. Bora Imani Children and Youth Foundation (BICYF)
11. Bright House of Change Organisation
12. Bright Vision Reform Tanzania
13. Bukoba Anti-Drugs Intellectually Organisation (BAIO)
14. Care for All
15. Community on Mental Wellbeing in Tanzania
16. Community Peers for Health and Environment Organisation
17. De Pores Memorial Foundation
18. Drug Abuse and Recovery Organisation (DARO)
19. Drug Abuse Prevention Initiatives Supporting Organization in Tanzania (DAPISOITA)
20. Empower care Foundation
21. Foundation for Community Involvement (FCI)
22. Foundation for Legal and Health Support
23. Gift Of Hope Foundation
24. Green Hope Organization
25. Health Aid and Care for the Future Foundation (HACFF)
26. Hope Community Reviver (HCR)
27. Jipe Moyo Centre
28. Juza Waste Pickers Initiative
29. Kibao Salama
30. Kibwena Community Development
31. Kimara Peers Educators and Health Promotors Trust Fund
32. Kirumba Movement for Harm Reduction
33. Konga Tabora
34. Life and Hope Rehabilitation Organization
35. Lindi Support Agency for Welfare
36. Mamas and Papas for Community Reform (MPCR)
37. Mapambano ya UKIMWI na Kifua Kikuu Temeke
38. Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA)

39. Methadone Recovery Community Empowerment Tanzania (MRCE-Tanzania)
40. Mtwara Non-Governmental Organization Network
41. Naweza Tena
42. Nazareth Choir
43. Next Generation Keepers Tanzania
44. Ngao ya Jamii
45. Nurget Development in Tanzania
46. Organization of Youth Against Risk Behaviours (OYARB)
47. Peers to Peers Supporting Group
48. People with Drug Dependency Relief Foundation
49. Pillimissanah Foundation
50. Purple Heaven Foundation
51. Recovery Brotherhood
52. Recovery Youth with Vision
53. Rondo Women’s Development Organisation
54. Round Table Ambassador of Change (ROTACHA)
55. Rukwa Association of Non-Governmental Organization
56. Saikolojia Sensitization Networking of Tanzania (SAIKO SENTA)
57. Secure Your Life Benefit Against Drug Addiction
58. Social and Economic Support for Drug Abuse Free Environment (SESDE)
59. Soma kwa Furaha Initiative (SKFI)
60. Steps Tanzania
61. Tandika Youth Rehabilitation and Handcraft Group (TAYOHAG)
62. Tanga Recovery Community
63. Tanzania Albinism Society
64. Tanzania Community Empowerment Organization (TCEO)
65. Tanzania Drug Prevention Network (TDPN)
66. Tanzania Health and Social Services (THSS)
67. Tanzania International Organization of Good Templars (T-IOGT)
68. Tanzania Network for People who Use Drugs (TANPUD)
69. Tanzania Organization of Good Templars (TOGT)
70. Tanzania Social Foundation for a Drug Free Generation
71. Waungwana Family
72. Women and Child Vision
73. Women Support Group
74. Wounded Healers Organisation
75. Youth Achievement Village in Tanzania (YAVT)
76. Youth and Community Rehabilitation (YCR)
77. Youth Empowerment and Psychotherapy Aid Organization
78. Youth Empowerment Society Tanzania (Yes-Tanzania)
79. Youth Volunteers Against Risk Behaviors (YOVARIBE)

Kiambata Na. II

Idadi ya Waraibu waliohudumiwa kwenye Nyumba za Upataji Nafuu "Sober Houses" kwa Mwaka 2024

Na.	Jina la Nyumba	Waraibu Waliohudumiwa		Mkoa
		Me	Ke	
1.	Arusha Recovery Sober House	97	0	Arusha
2.	Arusha Women Recovery Sober House	0	35	
3.	Njiro Women Recovery Sober House	0	60	
4.	Usa River Recovery Sober House	88	0	
5.	Surrender for Freedom Treatment Centre	125	0	
6.	Olmotonyi Recovery House	65	0	
7.	Moshono Foundation Sober House	80	0	
8.	Northern Hill Sober House	32	0	
9.	New Life Sober House	31	0	
10.	Tasor Sober House	119	0	
11.	Zayn Hope House	42	0	
12.	Meru Recovery Sober House	100	0	
13.	Vision of Hope Initiative	12	0	
14.	Changamoto ni Matumaini	67	0	Dar es Salaam
15.	Drug Abuse Prevention Organization (DAPO)	35	0	
16.	Dapo Women Recovery House	0	30	
17.	Drug Free Tanzania – The Right Way Recovery House	92	0	
18.	Drug Free Tanzania – The Ties that Bind us Recovery Center	65	0	
19.	Hope Again Rehabilitation and Wellness Foundation	42	0	
20.	MRCTanzania Kigamboni Sober House (1)	138	0	
21.	MRCTanzania Kigamboni Sober House (2)	69	0	
22.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (3)	74	0	
23.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (4)	103	0	
24.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (5)	49	0	

25.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (6)	34	0	
26.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (7) - Women Sober House	0	32	
27.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (8)	42	0	
28.	The Awaited Rehab Centre	21	0	
29.	Pillimissana Sober House	106	0	
30.	Pillimissana Women Sober House	0	8	
31.	Back to Life Sober House	2	0	
32.	Kilimanjaro New Vision and Sobriety 1	85	0	Kilimanjaro
33.	Kilimanjaro New Vision and Sobriety 2 (Women)	0	76	
34.	Kilimanjaro Recovery Home	47	0	
35.	Surrender for Freedom Treatment Centre (Njiapanda ya Himo)	69	0	
36.	Serenity Gate Rehab	56	0	
37.	Courage on Recovery Foundation	94	0	Tanga
38.	Gift of Hope Sober House	66	0	
39.	Gateway Sober House	10	0	
40.	Tanga Drug Free Organization	72	0	
41.	Kipepeo Foundation – Free at Last Sober House	57	0	Morogoro
42.	Cornerstone Recovery	63	0	
43.	New Vision of Life Society Sober House	147	0	Pwani
44.	Life and Hope Sober House	145	0	
45.	The Light of Miracle Organization - Women's Hope Rehabilitation	0	24	
46.	Mamaz and Papaz Sober House	28	0	
47.	Bagamoyo Sober House	200	0	
48.	Mapinga Sober House	06	0	
49.	Pillimissana Sober House	63	0	Mwanza
50.	MRC Mbeya Sober House	47	0	Mbeya
51.	MRC Kahama Sober House	07	0	Kahama
52.	Simama Tena Sober House	02	0	
53.	Foundation for Alleviation of Drugs Addiction and Suffering (FADAS)	22	0	Iringa
54.	Sobriety Forever Rehabilitation Centre	02	0	Kagera
55.	MRC Dodoma Sober House	24	0	Dodoma
	Jumla	**3,042**	**265**	
	Jumla kuu	**3,309**		

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya,
S.L.P 80327, 8 Barabara ya Kivukoni,
11486 Dar es Salaam Barua pepe: cg@dcea.go.tz
Tovuti: www.dcea.go.tz Instagram: @dceatanzania
Twitter: @dceatanzania Facebook: dcea_tz
YouTube: DCEATV Simu ya bure: 119